

**VIONGOZI KAMA VISABABISHI VYA MABADILIKO  
KATIKA RIWAYA ZA MWENDA MBATIAH: *VIPANYA*  
*VYA MAABARA NA MAJIRA YA TUFANI***

**NA  
ANNE WANGECI NJOROGE**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA  
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA IDARA  
YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2014**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine chochote

.....  
Anne Wangeci Njoroge  
Mtahiniwa

.....  
Tarehe

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi kupitia idara ya Kiswahili

.....  
Dkt. Tom Olali  
Msimamizi

.....  
Tarehe

.....  
Dkt. Evans Mbutia  
Msimamizi

.....  
Tarehe

## **TABARUKU**

Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu wapendwa marehemu Bw. Daniel Njoroge Macharia na mama yangu, Bi. Mary Nyakarura Njoroge kwa kunihamasisha nijitahidi kuboresha masomo yangu katika utu uzima.

## **YALIYOMO**

UNGAMO .....	ii
TABARUKU .....	iii
YALIYOMO.....	iv
SHUKRANI.....	vii
VIFUPISHO VYA MANENO .....	ix
IKISIRI .....	x

## **SURA YA KWANZA**

1.0 Utangulizi .....	1
1.1 Suala La Utafiti.....	1
1.2 Madhumuni ya utafiti huu .....	2
1.3 Maswali ya utafiti .....	2
1.4 Sababu za kuchagua mada hii.....	2
1.5 Msingi wa nadharia.....	4
1.6 Upeo na mipaka .....	8
1.7 Udurusu wa yalioandikwa kuhusu mada hii.....	8
1.8 Mbinu za utafiti.....	11

## **SURA YA PILI**

### **SUALA LA UONGOZI KATIKA AFRIKA YA MASHARIKI**

2.0 Utangulizi .....	13
2.1 Uongozi.....	15
2.2 Sifa za Uongozi Mzuri.....	16
2.3 Sifa za Uongozi Mbaya .....	16
2.4 Changamoto za Uongozi.....	18
2.5 Uongozi Barani Afrika .....	19
2.6 Uongozi Katika Afrika ya Mashariki .....	21
2.6.1 Uongozi Nchini Tanzania .....	22

2.6.2 Uongozi Nchini Kenya .....	26
2.6.3 Uongozi Nchini Uganda .....	29
2.7 Hitimisho .....	31

## SURA YA TATU

### UCHAMBUZI WA MAUDHUI NA WAHUSIKA KATIKA *VIPANYA VYA MAABARA*

3.0 Utangulizi .....	32
3.1 Muhtasari wa <i>Vipanya Vya Maabara</i> .....	33
3.2 Tathmini Ya Maudhui Kuhusu Makundi Ya Vipanya Vya Maabara.....	34
3.2.1 Mfumo wa Elimu wa 8-4-4.....	36
3.2.2 Vijana kama kundi la vipanya vya maabara .....	38
3.2.3 Tabaka la chini kama kundi la vipanya vya maabara .....	39
3.2.4 Ubaguzi wa Kikabila kama kundi la vipanya .....	40
3.2.5 Mataifa yanayoendelea kama kundi la panya wa majaribio .....	41
3.2.6 Watawaliwa kama kundi la vipanya .....	41
3.2.7 Njia tofauti kutumika kujinufaisha .....	42
3.3 Aina tofauti tofauti ya viongozi pamoja na mchango wao .....	43
3.3.1 Waziri Rashid Hamisi.....	43
3.3.2 Walimu kama viongozi katika asasi za Kielimu .....	46
3.3.3. Maofisa wa polisi.....	49
3.3.4. Wazazi kama viongozi nyumbani.....	51
3.4.Hitimisho .....	53

## SURA YA NNE

### UCHAMBUZI WA MAUDHUI NA WAHUSIKA KATIKA *MAJIRA YA TUFANI*

4.0 Utangulizi.....	55
4.1 Muhtasari wa <i>Majira ya Tufani</i> .....	55
4.2 Upambanuzi wa Maudhui Kuhusu Wananakada.....	56
4.2.1 Ukoloni na Ukoloni Mamboleo. ....	56

4.2.2 Ufisadi.....	59
4.2.3 Udhalimu kwa Wananakada. ....	62
4.2.4 Ubarakala au Ukabaila.....	65
4.2.5 Ukabila.....	68
4.3 Viongozi tofauti tofauti katika riwaya ya <i>Majira Ya Tufani</i> . ....	70
4.3.1 Balozi Dan Prince .....	70
4.3.2 Meya wa Nakada Macho Wa Tatu. ....	72
4.3.3 Kamishna wa polisi.....	73
4.4 Hitimisho .....	74

## **SURA YA TANO**

### **HITIMISHO**

5.0 Utangulizi .....	75
5.1 Muhtasari Wa Matokeo ya Utafiti .....	75
5.2 Tafiti za baadaye.....	79
<b>MAREJELEO</b> .....	80

## SHUKRANI

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote ambao walichangia ufanisi wa utafiti huu kwa njia moja au nyingine. Nimeamini kwamba umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

Kwanza kabisa, ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uwezo na siha njema katika safari hii ya kutimiza ndoto yangu ya kupata shahada ya uzamili na hasa wakati nilitafiti na kuandika tasnifu hii. Kukamilika kwa kazi hii kumetokana na ushirikiano nilioupata kutoka kwa watu mbalimbali huenda nisiwataje wote kwa majina, lakini ninawashukuru kwa njia ya pekee wasimamizi wangu; Dkt Evans Murage Mbutia na Dkt. Tom Olali ambao ushauri, maelekezo na tahakiki zao za kitaaluma zilinifaidi pakubwa na kuniwezesha kujua mengi ambayo kamwe singeyatambua.

Ninatoa shukrani zangu kwa wahadhiri wote katika taaluma ya Kiswahili na hasa wale niliotagusana na wao kupitia kwa mihadhara ya kozi ambao ni wafuatao: Mwenyekiti wa idara, Prof. John Habwe, Dkt Olali, Dkt. Mukhwana, Dkt. Swaleh, Prof. Abdulaziz, Prof. Mberia, Dkt. Buregeya, Dkt. Timammy, Prof. Kineene Wa Mutiso, Dkt. Zaja, Prof. Mbatiah, Dkt. Mbutia, Prof. Wamitila na Vilevile Shukrani Maalum kwake Prof. Aswani Buliba mhadhiri wa Chuo Kikuu Cha Laikipia aliyenifunza katika shahada ya kwanza chuoni Egerton kwa kunipevusha kuhusu NUHU.

Shukurani nyingine ziwaendee wasomi wenzangu tulioabiri meli hii tukasafiri pamoja na kutiana moyo hadi mwisho. Nao ni: Mary King'ora, Rose Merianga, Raitania Mwari, Josephine Emaita, Millicent Auko, Benjamin Kilanga na James Mburu.

Nawashukuru wazazi wangu marehemu Bw. Njoroge Macharia na Bi. Mary Njoroge na hasa mamangu aliyejitwika mzigo wa kumlea mwanangu wakati nimekuwa nikijishughulisha na masomo. Familia yote ya Njoroge naivulia kofia kwa mchango wenu, na shukrani za dhiti kwake dadangu Ruth Njeri na mumewe Muchemi kwa kunipa makao wakati nikisoma Mungu awajalie neema. Pamoja na hawa namshukuru mwanangu Gift Njoroge kwa uvumilivu wake wakati nilipokuwa nikisoma.

Nashukuru tume ya kuajiri walimu kwa kunipa likizo ya masomo iliyoniwezesha kuitimiza ndoto yangu. Likizo hii iliniwezesha kukazia masomo yangu bila majukumu mengi ya ufundishaji.

Mwisho ningependa kumshukuru Keziah Mwaura kwa kuipiga taipu kazi hii na kuhakikisha kwamba imekamilika katika wakati unaofaa. Kwa wale ambao sikuwataja kwa majina na walinfaa kwa njia moja au nyingine, nasema asante sana na Maulana awarudishie maradufu.



## **VIFUPISHO VYA MANENO**

NUHU	:	Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi
UHU	:	Uchanganuzi Hakiki Usemi
NRM	:	National Resistance Movement
AFP	:	Agence France Presse
UPC	:	Uganda People's Congress
CMC	:	Common Man's Charter
FBI	:	Federal Bureau of Investigation

## **IKISIRI**

Katika utafiti wetu tumeangazia viongozi kama visababishi vya mabadiliko katika riwaya za *Vipanya Vya Maabara* na *Majira Ya Tufani*. Jamii mbalimbali huwa na mitazamo anuai kuhusu majukumu ya viongozi na mchango wao hauwezi kupuuzwa. Mwandishi wa riwaya hizi ameangazia majukumu ya viongozi yanayoshabihiana katika kuleta mabadiliko kwenye jamii zake, hivyo basi makala haya yanachunguza mchango wa viongozi kama visababishi vya mabadiliko dhahiri. Tulichagua mada hii ili kuchambua riwaya hizi kwa sababu ya maudhui yanayoashiria jinsi hali halisi ilivyo katika jamii zetu. Malengo ambayo tumeyaangazia ni kuchunguza jinsi matendo ya viongozi yanavyohujumu uchumi wa nchi, kutathmini ikiwa matendo ya viongozi yanaakisi maadili ya kijamii na kupambanua hali za unafiki zinazodhihirika katika matendo ya viongozi.

Tulijikita kwenye kazi hizi mbili *Vipanya Vya Maabara* na *Majira ya Tufani* pamoja na kurejela kazi zingine ili kutoa idhibati zaidi. Tuliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi iliyoasisiwa na Norman Fairclough, Teun Van Dijk na Ruth Wodak miongoni mwa wengine, kwa mitazamo ya Wodak na Reisigl, inayozingatia mkakati wa kurejelea, mkakati wa unominishaji, mkakati wa ubishi, mkakati wa kudhihirisha nguvu za usemi na vilevile mkabala. Baadhi ya mambo yaliyojitokeza katika utafiti wetu ni kwamba mabadiliko yanayoshuhudiwa katika nchi na jamii mbalimbali husababishwa na viongozi. Kwa mfano ufisadi, utabaka, wizi wa kimabavu, hujuma miongoni mwa maovu mengine mengi. Mabadiliko haya yanasababishwa na kuweko kwa uwezo mkubwa wa watawala katika kuwatawala watawaliwa.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumeshugulikia: Usuli wa mada ya utafiti, suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada ya utafiti huu, udurusu wa yalioandikwa katika viwango mbalimbali vya usomi ambayo yanahusiana na utafiti huu na pia yale yanayohusu nadharia ya uchanganuzi hakiki usemi (NUHU) kwa jumla. Aidha tumeeleza njia mwafaka zitakazotumika katika utafiti huu tukitamatisha sura yenyewe na umuhimu wa utafiti wenyewe.

## 1.1 Suala La Utafiti

Viongozi katika jamii yoyote ile au taifa kwa jumla, huwa na majukumu muhimu sana. Mchango wao hauwezi kupuuzwa. Wao ndio hutumika kama mawakala wa mabadiliko chanya katika jamii. Utafiti huu hivyo basi ni jaribio la kuhakiki mchango wa viongozi kama visababishi vya mabadiliko dhahiri katika riwaya za Mwenda Mbatiah . Kuliziba pengo hili, utafiti huu umechunguza na kuchanganua namna ambavyo nyendo zao, matendo yao au maneno yao yanavyochochea au kudumaza mabadiliko katika jamii za *Vipanya Vya Maabara* na *Majira Ya Tufani*. Tutatumia misingi ya nadharia ya uchanganuzi hakiki usemi ambayo kwa hakika haijatumika sana katika uwanja huu kuchanganulia matini ndefu.

Ndiyo sababu utafiti wetu utamulika maswala kama vile matendo ya viongozi yanayoweza kusababisha hujuma kwa wanajamii, kuvuruga maadili ya kijamii na kudhihirisha unafiki.

## **1.2 Madhumuni ya utafiti huu**

Kazi yetu itaongozwa na madhumuni yafuatayo:

- i) Kuchunguza matendo ya viongozi yanayohujumu uchumi wa nchi.
- ii) Kutathmini ikiwa matendo ya viongozi yanaakisi maadili ya kijamii.
- iii) Kupambanua hali za unafiki zinazodhihirika katika maneno na matendo ya viongozi.

## **1.3 Maswali ya utafiti**

Utafiti huu utaongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

- i) Je, matendo ya viongozi yanaweza kuhujumu uchumi wa nchi?
- ii) Je, matendo ya viongozi yanaweza kuakisi maadili ya kijamii?
- iii) Je, maneno na matendo ya viongozi aghalabu yanaweza kudhihirisha unafiki wao?

## **1.4 Sababu za kuchagua mada hii**

Baadhi ya sababu zilizochangia katika kuteuliwa kwa mada hii ni pamoja na hizi zifuatazo:

Kwanza kabisa, matini zinazoshughulikiwa katika utafiti huu ambazo ni *Vipanya Vya Maabara* na *Majira Ya Tufani*, riwaya za Mwenda Mbatiah hazijawahi kuhakikiwa katika misingi ya nadharia ya uchanganuzi hakiki usemi na kwa hivyo utafiti huu unadhamiria kuziba pengo hili. Mwandishi wa matini hizi mbili ni mwandishi aliyetoa mchango mkubwa katika Fasihi ya Kiswahili na ameandika kazi nyingi zaidi ambazo zimevutia uchunguzi wa kiakademia kwa kiwango kikubwa kwa hivyo tulitaka kujua jinsi riwaya hizi zinavyoweza kuwasilishwa kwa mtazamo wa nadharia ya uchanganuzi hakiki usemi.

Katika baadhi ya kazi zake kama vile *Wimbo Mpya* (2004) na *Upotevu* (2005) Mbatiah anazungumzia mabadiliko yanayohusu jamii kama vile:Ufisadi, ukoloni mamboleo, unafiki, ukombozi, umaskini, uhuru, utu na utajiri na mengineyo. Kwa hivyo tunataka kujua ikiwa baadhi ya mabadiliko haya yanajitokeza katika *Vipanya Vya Maabara* na *Majira Ya Tufani* na ni vipi viongozi wanasababisha mabadiliko hayo.

Kwa sababu katika uwanja huu wa Kiswahili hapajakuwa na uhakiki wa riwaya hizi kwa mtazamo tuliouteua, tumeona ni muafaka kuzishughulikia, kwani kila wakati viongozi huonekana kama vielelezo vyema vya kuigwa, ni muhimu kuwa na tafiti za aina hii ili kuipasha jamii ya sasa habari kuhusu mienendo ya viongozi wetu.

Mada hii itafaa sana hasa kwa wakati huu ambapo nchini Kenya ufiisadi na dhuluma kwa wanyonge unapigwa darubini ili kusitishwa, hii ni kwa mujibu wa Katiba mpya ya Kenya (2010) sura ya sita sehemu ya sabini na tatu, ibara ya pili kipengele cha (b) ambapo ufiisadi unaangaziwa. Aidha itatuwezesha kutoa mchango wetu ili kufikia njia mwafaka za kukabiliana na changamoto za uongozi.

Sababu nyingine iliyochangia katika kuteuliwa kwa mada hii ni mtazamo wa mwandishi kuhusu viongozi na uongozi wao katika Ulimwengu Wa Tatu hususan bara la Afrika na uhusiano wao na Ulimwengu Wa Kwanza, yaani mataifa ya Magharibi na uongozi ambao unaonekana kuwa na uwezo mkubwa ambao unastahili kudhibitiwa ili kupunguza mchango wao katika uozo wa jamii.

## **1.5 Msingi wa nadharia**

Katika utafiti huu tunaongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi (NUHU).Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi imeasisiwa na Norman Fairclough, Teun Van Dijk na Ruth Wodak miongoni mwa wengine. Utafiti unaongozwa na mitazamo ya Wodak na Reisigl (2001).

Kwa mujibu wa Van Dijk (1998) Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU) ni taaluma inayohusu uchunguzi na vilevile uchanganuzi wa matini na misemo ili kutambua hoja maalumu kuhusu chanzo cha uwezo, ukandamizwaji, utofauti (kutokuwa sawa) na upendeleo. UHU hutathmini jinsi vyanzo hivi maalumu vinavyodumishwa na kutolewa upya ndani ya muktadha wa ushirikiano maalumu, Kisiasa na Kihistoria. Vilevile katika Van Dijk (2008:85) tunaelezwa kwamba UHU ni aina ya uhakiki unaotafiti kwa kiasili jinsi dhuluma za uwezo wa kijamii, ukandamizwaji na kutokuwa sawa unavyobuniwa na kutolewa upya na vilevile kupingwa kwa matini na misemo katika muktadha wa kijamii na kisasa.

Kwa mwelekeo sawa na huu, Fairclough (1993)) anafasili Uchanganuzi Hakiki Usemi kama:

Uchanganuzi hakiki ambao unatalii kwa utaratibu mahusiano ya visababishi ambavyo mara kwa mara havieleweki na kuamua baina ya (a) Mazoea yasiyo na msimamo, matukio na matini, pamoja na (b) Mahusiano mapana na miundo ya tamaduni, mahusiano na namna; kupeleleza jinsi mazoea haya, matukio na matini hutokea na kujengeka kiitikadi na mahusiano ya uwezo pamoja na mapambano kuhusu uwezo; na kutalii jinsi utata wa mahusiano haya kati ya usemi na jamii hasa huwa sababu za kudumisha uwezo na mamlaka. (uk 135)

(Tafsiri yetu)

Kwa kawaida, uchanganuzi hakiki usemi hulenga katika kuweka wazi desturi za mahusiano baina ya desturi za usemi, desturi za ushirikiano na vilevile desturi za miundo, mahusiano ambayo hayangeeleweka kwa mtu wa kawaida.

Katika Uchanganuzi Hakiki Usemi, kuna mikakati mitano ifuatayo:

1. Mikakati wa kurejelea
2. Mikakati wa unominishaji
- 3 Mikakati wa ubishi
4. Mikabala
5. Mikakati wa kudhihirisha nguvu za usemi.

Mambo haya matano yanashabihiana na maswali matano yafuatayo.

1. Je, watu huwarejelea wengine namna gani kiisimu?
2. Ni sifa gani, hulka gani na dhamani gani ambazo huwa zinapewa watu?
3. Ubishi huwa unaendelezwa kupitia mikakati gani? Yaani ubaguzi, uonevu, ukandamizwaji huendelezwa namna gani?
4. Mikabala gani hudhihirika?
5. Je, usemi husika una uzito gani? Ni ya majazi ama umefichwa kidogo?

Utafiti huu, utatumia baadhi ya mikabala hii katika kuchanganua riwaya mbili za Mwenda Mbatiah. Fairclough na Wodak (1997) wanapendekeza mtazamo wa Uchanganuzi Hakiki Usemi (UHU) katika kufafanua mifanyiko ya kijamii ambayo inazalisha matini, na mifanyiko ya kijamii ambamo wanajamii au watu wanazalisha maana katika mawasiliano katika usemi. Nguzo za Uchanganuzi Hakiki Usemi ambazo zinahusiana na utafiti huu ni mtagusano.

- Mahusiano kila mara huhusiana na uwezo na itikadi.
- Kila tukio la mawasiliano linahusu uchanganuzi wa aina nyingi Wodak and Ludwig, (1999:12-13).

Nguzo ya kwanza inaelekeza kwamba palipo na mtagusano, mahusiano ya njia fulani huwepo. Kwa mfano, uhusiano na uwezo. Pili usemi unahusiana na njia nyingine za matukio ambazo hutendeka kwa pamoja au yaliyotendeka awali. Vilevile, kuna uwezekano wa kuwa na aina nyingi za uchanganuzi. Matukio ya mawasiliano hutegemea mitazamo ya wahusika na kiwango cha uelewa. Utafiti huu utaangazia uhusiano wa kijamii ambao unaweza kuruhusiwa katika usemi wa wanajamii. Fairclough na Wodak (1997), wameweka wazi kwamba usemi unajumuisha taarifa, utambulisho wa jamii na mahusiano ya kijamii kati ya vikundi vya watu. Hili linamaanisha kwamba katika kila usemi ufahamu, utambulisho wa jamii na mahusiano ya jamii yanaanzishwa na kuundwa upya. Uchanganuzi Hakiki Usemi unakiri uwezo kama jambo lenye maana katika uundaji wa usemi. Uchanganuzi Hakiki Usemi unamulika mahusiano ya uwezo kati ya wahusika tofauti katika jamii.

Uhusiano huu una msingi wake katika utawala. Kikundi kimoja ni cha utawala ilhali kile kingine kinatawaliwa. Wakati mwingi, watu wenye uwezo hutumia uwezo wao kutawala wengine. Matumizi haya mabaya ya uwezo ndilo jukumu maalum la uchanganuzi hakiki usemi. Ni jambo linalokubaliwa kwamba lugha, kivyake haina uwezo. Hata hivyo lugha hupata uwezo kupitia jinsi ambavyo wale wenye uwezo hutumia lugha hii. Matumizi haya hujumulisha vile vile matini ndefu kwa mfano riwaya. Van Dijk (1997) anaeleza kwamba kuna matumizi mabaya ya uwezo kwa wenye uwezo kupitia usemi kama njia ya kitega uchumi kiitikadi.



Uchanganuzi hakiki usemi inatarajia kwamba wale wanaotawaliwa watie bidii kujinusuru kutoka kwa watawala. Kama suluhisho inatarajiwa kwamba wanaotawaliwa wakaidi. Ukaidi huu huenda usifaulu lakini kilicho muhimu ni kule kuwepo kwake.

Itikadi ni nguzo muhimu katika UHU. Itikadi inahusu kuwaweka watu katika kikundi fulani na kwa njia fulani kama kikundi cha nafasi fulani katika jamii. Inaonyesha ukweli wa jamii kuhusu watu fulani ama jamii ambamo wanaishi. Karibu kila wakati ni kweli kwamba matakwa ya wenye uwezo kijamii hudumu. Itikadi zimewekwa kwenye akili katika mazoezi ya usemi kwa namna tofauti tofauti za ishara.

UHU sio njia ya moja kwa moja, idara, au namna maalumu inayofuata mitazamo mingine mingi katika uchunguzi wa usemi, bali hunuia kutoa namna au taswira tofauti ya kutoa nadharia, uchanganuzi na utekelezaji popote kwenye taaluma yeyote. Tunaweza kupata taswira nyingi au chache za hakiki katika maeneo anuwai kama Pragmatiki, Uchanganuzi wa mazungumzo, Uchanganuzi wa masimulizi, Balagha, Elimu mitindo, Isimu jamii, Ethnografia, Uchanganuzi wa vyombo vya habari au njia za mawasiliano baina ya zingine nyingi (Van Dijk, 2008:85 )

Dijk (2008) pia alieleza kwamba la muhimu sana kuhusu UHU ni utambuzi dhahiri wa nafasi yake kwa jamii kuendeleza desturi ambazo zinakataa uwezekano wa sayansi ya thamani huru, na hasa usemi wa kitaaluma, ni sehemu asilia ya mahusiano na huathiriwa na miundo ya mahusiano na hutolewa katika mtagusano wa mahusiano.

Jukumu lingine la UHU ni uhakiki wa kina. Nia hasa ni kuweka usemi wazi kwa kuvumbua kwa undani kaida ambazo ni kinzani na ambazo zimeunda ushindani wa itikadi na uwezo katika matini. UHU pia inachunguza maana halisi na dhanio katika matini au usemi. Maana

hujitokeza wakati ambapo mazungumzo au maandishi humaanisha zaidi ya yale ambayo wanayoyasema au kuyaandika. Hivi ni kusema kwamba ni maana iliyodokezwa kuhusu utungo, ambayo hutolewa katika muktadha wa matumizi. Dhanio huibuka wakati ambapo wazungumzi au waandishi hudhania kwamba msikilizi au msomaji atapokea lile ambalo linawasilishwa bila kutilia maanani. Hili linamaanisha kwamba wawasilishi wa ujumbe huchukulia kwamba wako katika makubaliano na wapokeaji wa ujumbe katika yale ambayo yanasemwa ama kuandikwa (wamo katika dau moja).

### **1.6 Upeo na mipaka**

Utafiti huu unanua kuchunguza matendo ya viongozi ambayo huhujumu uchumi wa jamii, kuyatathmini ikiwa yanaakisi maadili ya kijamii na kuchunguza jinsi yanavyochangia katika kuleta mabadiliko kwenye jamii.

Tutajihusisha na kusoma *Vipanya vya Maabara* na vilevile *Majira ya Tufani*, tukichanganua vipengele vya dhamira na maudhui ili kutambua matendo na maneno ya viongozi na kuona jinsi yanavyoathiri jamii zao. Kazi hizi tumeziteua kama sampuli tu kwa sababu zinatupatia data tuihitajiyo katika tathmini yetu na zimeakisi hali ilivyo kwenye jamii ya sasa na hasa jamii ya Kenya. Licha ya hayo muda tulio nao hauturuhusu kuziangalia kazi zote zinazomulika suala hili. Hata hivyo hatutasita kuzitaja kazi zingine hasa za Mbatiah ili kutilia mkazo hoja fulani katika tathmini yetu.

### **1.7 Udurusu wa yalioandikwa kuhusu mada hii.**

Utafiti huu ni tokeo la tathmini za tafiti mbalimbali zilizoshughulikia namna mbalimbali za mabadiliko kwenye jamii hususan wale wanyonge na vilevile vijana. Katika kazi hizo zote kuna wazo kwamba jamii inabadilika kwa njia hasi au chanya lakini sababu hasa za mabadiliko hayo haziangaziwi. Tasnifu yetu imelenga kuliziba pengo hilo kwa kutathmini

viongozi kama visababishi vya mabadiliko katika *Vipanya vya Maabara* na *Majira ya Tufani*.

Baadhi ya tafiti zilizogusia suala hili la mabadiliko katika jamii ni:

Mugambi (1983), alihakiki Kilio cha wanyonge katika riwaya za Said Ahmed Mohamed zifuatazo: *Asali Chungu* (1978), *Utengano* (1980) na *Dunia Mti Mkavu* (1980). Anapotuonyesha jinsi wanyonge wanavyodhalilishwa na jamii, mahusiano na kazi yetu ni kwamba inatupa uelewa mzuri wa mabadiliko hasi yanayotolewa na viongozi katika jamii ya *Vipanya Vya Maabara* hususan kwa vijana. Aghalabu tunapata kufahamu ni kwa vipi suluhu zingefikiwa kwa urahisi katika kutatua janga la dhuluma. Mhakiki huyu katika kuhakiki wahusika huku akiangazia sifa zao, anatupatia mfano mzuri wa kiongozi Bw. Meksuudi ambaye kwa kumtumia Kazija anatumulikia hizaya za Bw. Meksuudi, pale ambapo anasema kwamba Meksuudi anageuza haki kuwa haramu, na tamu kuwa chungu. Vilevile anaonyesha jinsi Meksuudi anavyowaongoza watu katika maangamizi badala ya kuwaongoza katika haki na mema.

Kiongera (2012), alishughulikia mchango wa vijana kuleta mabadiliko chanya katika tamthilia chache za Kiswahili zifuatazo: *Kifo Kisimani Wa Mberia K.* (2001), *Pango Wamitila K. W.* (2003), *Maua Kwenye Jua la Asubuhi Wa Mberia K.* (2004) na *Seserumbe Wamitila K.W.* (2009). Hata ingawa mhakiki huyu alitumia tamthilia kuonyesha mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya, haya yatatufaa zaidi kwani kinyume cha chanya ni hasi na bila shaka mawili hayo huambatana. Tutaweza kutambua mabadiliko hasi kwa urahisi. Mtunzi wa kazi hii alitumia nadharia ya Ki-Foucault inayohusishwa na Michael Foucault, mwananadharia wa Kifaransa, angalau itatupa fursa ya kutambua jinsi watu huweza kuathiriana katika mtagusano na maingiliano yao na kudhihirisha kwamba kila mtu katika jamii huwa na mamlaka yake.

Manoti (2012), alishughulikia dhamira ya uozo na athari zake kwa jamii katika *Upotevu* (2005). Mtunzi wa kazi hii anafafanua kwa undani dhamira ya uozo katika riwaya ya *Upotevu* na kuonyesha kinaga ubaga jinsi mwandishi wa riwaya hii alivyosawiri jamii husika. Aidha alionyesha jinsi mtunzi wa riwaya hii alivyobainisha uozo katika jamii yake kwa uwazi na ukamilifu, hali ambayo imetuwezesha kutambua chanzo cha mabadiliko hasi katika riwaya za *Vipanya Vya Maabara* na *Majira ya Tufani*.

Naliaka (2012), naye katika kazi yake alishughulikia Uhakiki wa hali ya vijana katika *Vipanya Vya Maabara*. Katika utangulizi wake alieleza kinaga ubaga matatizo yanayowakumba vijana katika jamii na chanzo cha changamoto ambazo zinawakumba. Kwa mfano, anaeleza kwamba chanzo cha Muli kubobea madawa ya kulevya ni kukosa baba mzazi wa kumwelekeza ambaye kwa maoni yetu ndiye kiongozi pale nyumbani. Vilevile baba yao Bob na Freda anajitosa kwenye ulevi na kutupilia mbali majukumu yake. Sababu za mzazi huyu kufanya hivyo ni kwamba hasira zimemzidi kwa kutopandishwa cheo anachostahili pale kazini, hali ambayo inadhihirisha ufisadi unaochangiwa na viongozi.

Aidha mhakiki huyu aliwahakiki wahasika wote huku akiangazia chanzo cha changamoto zinazowakumba lakini kwa wepesi tu. Sisi tunatarajia kuangazia kwa undani ili kutathmini hasa chanzo cha maendeleo hasi ya jamii husika. Aghalabu katika sura ya nne alihakiki maudhui kuhusu vijana. Alitaja yale yaliyo hasi na vilevile yale chanya katika jamii, sisi tunatarajia kuangazia chanzo cha shida zenyewe. Kazi hii bila shaka itatufaidi pakubwa katika kuangazia maudhui kwa sababu ndiyo yatakayotuongoza katika kuteua mchango wa viongozi katika kuleta mabadiliko katika jamii ya riwaya za Mwenda Mbatiah.

Mawazo na maoni haya ya Naliaka pamoja na wahakiki wengine tuliowateua yana uhusiano mkubwa na utafiti wetu tunaoufanya kwa sababu yametaja baadhi ya mambo tunayoshughulikia katika kazi hii. Tofauti iliyopo ni kuwa nadharia tuliyoiteua ya uchanganuzi hakiki usemi ni tofauti na zile walizozitumia na huenda itafaa zaidi katika kutafiti kazi hii na kutuwezesha kuibua changamoto za uongozi na njia mwafaka za kukabiliana na changamoto hizo jambo ambalo hawakulifikia.

### **1.8 Mbinu za utafiti**

Utafiti wetu kimsingi ni uhakiki wa maktabani ambao umehusu kusoma na kuzihakiki riwaya na hata kuweza kusoma baadhi ya riwaya zingine za Mwenda Mbatiah ili kupata mwelekeo wa uandishi wake ambazo ni; *Upotevu* (2005), na *Wimbo Mpya* (2004). Vilevile tumesoma riwaya za Ahmed Mohamed zifwatazo; *Asali Chungu* (1978), *Utengano* (1980), na *Dunia Mti Mkavu* (1980) ili kuweza kuelewa jinsi wanyonge wanavyodhalilishwa.

Vilevile tumesoma tamthilia chache za Kiswahili zifwatazo; *Kifo Kisimani* (Wa Mberia 2001), *Pango* (Wamitila 2003), *Maua Kwenye Jua la Asubuhi* (Wa Mberia 2004), *Seserumbe* (Wamitila 2009) ambazo zimetupa ufahamu wa mchango wa vijana katika kuleta mabadiliko chanya katika tamthilia hizo ambao umetufaa katika utafiti wetu. Kadhalika tumezipitia tasnifu mbalimbali zinazohusiana na maudhui ya utafiti wetu na kupata ufahamu wa mada yetu.

Tumewahusisha wataalamu mbalimbali na wasanii ambao wametupa mwanga kuhusu maswala mbalimbali ambayo yametufaidi katika utafiti huu. Tumetumia mitandao mbalimbali kwenya tovuti hasa kuhusiana na maswala ya viongozi, uongozi, unyanyasaji, ufidadi na pale

tulipohitajika ufafanuzi na mwelekeo wa karibuni, hususan katika eneo la nadharia ya uchanganyuzi hakiki usemi.

## SURA YA PILI

### SUALA LA UONGOZI KATIKA AFRIKA YA MASHARIKI

#### 2.0 Utangulizi

Katika sehemu hii, tumerejelea kwa ufupi usuli wa viongozi na mifumo tofauti tofauti ya uongozi ili kuonyesha kwamba pana umuhimu wa kujaribu mifumo badilia ya uongozi ili kuleta mabadiliko yanayofaa kwa jamii. Pamoja na hayo tumesainisha sifa za uongozi mzuri na vilevile uongozi mbaya, tukiangazia changamoto zinazowakumba viongozi. Sura yenyewe ina umuhimu mkubwa katika kuelewa ni kwa namna gani viongozi huweza kuchangia katika mabadiliko kwenye jamii.

Mbali na kuupitia uongozi Barani Afrika hususan Afrika ya Mashariki kuhusu maendeleo na uwezo wa viongozi katika kuchangia katika maendeleo hayo, tumegusia mchango wa mataifa ya magharibi na athari zake katika viongozi wa Afrika kwa ujumla.

Kiongozi ni mtu anayesimamia na kueleza watu au kikundi cha watu (wanajami) ili wafanye kazi au shughuli fulani kwa njia inayostahili. Kwa ufupi kiongozi huwaongoa watu katika kutenda mema kwa njia ya haki na ya kuridhisha. Katika *Vipanya Vya Maabara* (2007) na *Majira Ya Tufani* (2012) tuna aina tofauti tofauti za viongozi, kwa mfano, tuna viongozi wa serikali, wabunge, wazazi wa kiume na vilevile wa kike baina ya wengine.

Viongozi na jamii zao wanajitahidi juu chini kutambuliwa na kujitawala huku wakisababisha mgawanyiko mwingi ulimwenguni. Umoja wa mataifa ulipoanzishwa ulikuwa na mataifa 51, leo una mataifa 191.

Ijapokuwa jitihada za kuleta mabadiliko zimezungumziwa sana, hatujaona mabadiliko makubwa. Licha ya jitihada za watu wengi wenye nia nzuri, kwa nini wananchi wameshindwa kuleta mabadiliko hata katika karne hii ya ishirini na moja?

Swali kama hilo lilijibiwa kwa sehemu na mmoja kati ya mawaziri wakuu waliohudhuria ule mkutano wa ushirikiano wa kiuchumi. Alisema hivi, “kuna jambo hili linaloitwa Utaifa naam, wanadamu wamelewa Utaifa. Kila taifa na kabila linachochewa na tamaa ya kujitawala na roho ya mashindano na pupa hufanya mambo yawe mabaya zaidi. Viongozi hufanya masilahi yao kuwa ya muhimu kuliko ya wananchi.” \*

Hata baada ya uhuru kupatikana viongozi walioshika hatamu hawakubuni sera kabambe kuweza kushughulikia hususan maendeleo ya jamii na hili ndilo chanzo cha shida za mabadiliko zinazotukumba.

Waandishi wengi wa Kifasihi katika maandishi yao ya hapo awali hawakuzingatia sana mchango wa viongozi katika mabadiliko na hata kazi chache zilizoandikwa kuhusu viongozi ziliangazia maendeleo chanya yaliyoletwa na viongozi, huku yale hasi yakiwa nadra mno.

Leo hii nchini Kenya waandishi wasomi wameanza kuangazia maswala ya viongozi na majukumu yao. Riwaya za *Vipanya Vya Maabara* na *Majira Ya Tufani* ni baadhi ya kazi ambazo zimeangazia kwa kina matendo, maneno na nyendo za viongozi ambazo zinachangia sana katika kusababisha mabadiliko katika riwaya hizo.

---

\* Jibu kutoka kwa waziri kuhusu ulimwengu kukosa umoja



## 2.1 Uongozi

Uongozi mzuri au uongozi mbaya si dhana rahisi kufafanua, hata hivyo kuna wazo la kijumla linalokubaliwa kuhusu yanayohusiana na uongozi mzuri. Ochola (2009) akirejelea De Laspirit des loi anaeleza kwamba, Montesqueieu anaweka tofauti baina ya aina tatu za serikali kulingana na utaratibu wake wa kimsingi kwa kusema kuna mifano tofauti ya uongozi, kwamba:

Mfano wa kijamhuri ambapo watu wote au sehemu yao ina nguvu za utawala, mfano wa kifalme ambapo mtu mmoja hutawala lakini kwa mujibu wa sheria zilizowekwa na kuelezwa kwa uwazi, na vilevile mfano wa kidikteta pale ambapo mtu mmoja pasipo na kujali kuhusu sheria na kanuni hutenda kama apendavyo, kwa kuangalia nia au haja zake . Fedel Castro (1968:85)

(Tafsiri yetu)

Kwa hivyo ni jambo la kimaantiki kulingana na maoni haya kufikia uamuzi kwamba, kiongozi mzuri ni yule anayeongoza kwa idhini ya anaowaongoza na hutumia msimamo wa mashauriano kufikia uamuzi wa kile kinachokubalika na wengi. Kwa ufupi kiongozi mzuri hujumuisha misingi ya uongozi wa kidemokrasia. Mwandishi wa Ufaransa Francis Hotman katika Ochola (2007), hudai kwamba kuna mkataba au mapatano kati ya serikali na wahusika wake, na kwamba watu wanaweza kuzua uasi dhidi ya utawala wa kimabavu au udhalimu wa serikali wakati serikali zinakiuka makubaliano hayo.(Ochola, 2007:16)

## **2.2 Sifa za Uongozi Mzuri**

Kulingana na Ochola (2007:18), kwa jumla uongozi mzuri ni uongozi ulio na baadhi ya sifa zifuatazo; Uwezo au nafasi ya kudumisha amani katika taifa, sheria na utulivu ambazo ndizo sifa muhimu katika utenda kazi wa viongozi; Uwezo wa kudumisha amani ya taifa ili kuwaweka wananchi wake katika hali ya usalama, ya usawa mbele ya sheria, na mahali ambapo hakuna mtu aliye juu ya sheria; Uwezo wa kutovumilia wanaotumia uwezo wao kiholela, lakini kuwa na uwezo wa kuhimiza utaratibu wa kufanya jambo kwa njia ya kuhakiki ili kuzuia matumizi mabaya ya madaraka, na uongozi ambao hukuza njia za kufanya maamuzi ambayo ni ya wazi, yanayoweza kukisiwa na vilevile yanayoweza kutegemewa kwa uaminifu wa hali ya juu; Uwezo wa kugundua na kukabiliana na ufiadini pasipokujali umaarufu na cheo cha wenye hatia; Uwezo wa kuweka nidhamu za ushirikiano; Na vilevile uwezo wa kukuza ushirikiano unaopendwa katika uongozi na maendeleo kwa jumla.

## **2.3 Sifa za Uongozi Mbaya**

Kwa upande mwingine uongozi mbaya huwa na sifa ambazo ni kinyume na sifa za uongozi mzuri. Were (1983) historia ya Afrika huru inatambulika kwa mwelekeo unaoshikiliwa na viongozi wa kimataifa na serikali kupuuza umuhimu na ufaafu wa maadili ya umma katika matendo na mienendo, na matendo ambayo yanaonyesha kana kwamba nchi zao na rasimali za mataifa yao ni vitu vidogo vikilinganishwa na maisha yao ya kibinafsi na mali ya familia zao.

Katika hali kama hizi jamaa zao, marafiki na kabila lao kawaida hupewa nyadhifa za juu katika uongozi na vilevile mishahara mikubwa pasipo kujali ustahili. Jinsi Forje alivyoadili katika Were (1983) kwamba wananchi wa kawaida katika nchi nyingi za Afrika huishi

maisha mafupi duni ambayo sio ya kuvutia kushinda yale ya mababu zao ilhali Afrika ndilo bara tajiri sana duniani kwa upande wa madini na rasilmali. Kwamba viongozi hukosa miundo misingi ya kuandaa wanadamu, badala yake wanawatumia kama mifereji ya kuendeleza unyanyasaji, kutajirika kwa muda mfupi sana kwa kutumia njia yeyote ile.(Were, 1983:8) Kwa ufupi sifa za uongozi mbaya hudhihirika kwa kukosa mwelekeo unaofaa.

Hali hii bila shaka inajitokeza katika *Vipanya Vya Maabara*, na *Majira ya Tufani*, ambazo zimeangazia kikamilifu matatizo yanayozikumba jamii zake. Kama vile ukabila, dhuluma, ufisadi, ubakaji baina ya mengine mengi na yanayochangia katika mabadiliko hasi katika riwaya hizo. Mandhari yaliyotumiwa katika *Vipanya Vya Maabara* ni ya jiji la Nairobi na viunga vyake, matatizo na changamoto zinazowakumba wanajamii hao ni hakikisho nzuri sana la hali ya maisha katika taifa letu kwa jumla. Kwa mfano kuna makundi tofauti ya vipanya vya maabara yanayotumiwa na viongozi katika kufanyia majaribio. Baada ya tafiti zao makundi hayo yanatupiliwa mbali na hata kuangamizwa bila hata kujali hali yao maishani. Mfano mzuri ni pale ambapo waziri Rashidi Hamisi anapotumia vijana kama soko lengwa kwa kuwaingiza vijana kama vile Swaleh katika biashara ya kumuuzia madawa ya kulevya kisha Swaleh anaathirika maishani.

Katika *Majira ya Tufani*, Mheshimiwa Meya, Macho wa Tatu ananyakuwa ardhi ya wakazi wa Nakada ambayo imetengewa umma na kujenga jengo kubwa la kimaarufu analoliita MACHO PLAZA badala ya kujenga Chuo Cha Uhasimu ambacho kingelea mafunzo ya dini na pia kazi mbalimbali kwa Wananakada. Kiongozi huyu anawapumbaza Wananakada kwamba jengo hilo ni la umma na litawafaa na vilevile ni fahari ya jiji la Nakada. Kiongozi huyu anatumia mamlaka ya umeya kubadilisha hati za umiliki wa kile kiwanja cha ekari mbili ambapo Macho Plaza inasimama kwa mikogo, kisha anatia

mfukoni mamilioni ya pesa za haramu zinazotokana na kodi ya jumba hilo. Hali kama hii ya kupora mali ya umma imekithiri katika ulimwengu wa tatu ikipelekea mwananchi wa kawaida kubakia katika lindi la umaskini na ufukara.

## **2.4 Changamoto za Uongozi**

Baadhi ya changamoto za uongozi kulingana na Were (1983) ni kwamba, tafiti zilizofanywa kuhusu ufisadi baina ya mataifa ya Afrika, zinaonyesha changamoto za aina nyingi. Katika changanuzi za Ronald Wraith na Edgar Simpkins (1964) waliona umaskini ndiyo sababu hasa ya kuenea kwa ufisadi baina ya changamoto zingine. Ukosefu wa desturi zinazofaa hasa miongoni mwa viongozi zilitambulika vilevile kama sababu kuu za ufisadi. Walizidi kusema kwamba, viongozi huoreshwa kwa urahisi kwa sababu wao sio warithi wa desturi za hifadhi za majukumu ya umma.

Mbali na umaskini pamoja na ukosefu wa viongozi wa sifa nzuri, wanaamini kwamba changamoto zingine za uongozi ni desturi za Kiafrika za ukarimu na kupeana zawadi; uzembe; uchangukaji wa thamani za desturi na kiwango cha maadili ambao kwa bahati mbaya haujafidiwa kwa njia mwafaka kwa kutumia njia tofauti za Kimagharibi; na mzigo mkubwa wa jamaa zao za Kiafrika. Changamoto hizi ndizo hasa zinazochangia katika shinikizo la uhitaji kwa viongozi na kuwalazimu kuishia katika ufisadi au maovu ili kuendelea kuishi. Hivyo basi inawalazimu kujiingiza katika ufisadi au maovu ili kuendelea kuishi na kuwalazimu kutumia ushawishi ili kuwawezesha wanajamii wao kupata ajira mathalani wangebakia kuwa mzigo wa daima kwao iwe popote pale.

Kwa mfano katika kongamano la baraza lilohusu changamoto zinazowakumba viongozi katika maendeleo ya Afrika huko Naijeria, rais wa awali wa Naijeria Babangida alieleza kuwa katika mwisho wa robo ya karne ya 20, Afrika inajipata katika madeni yaliyosalia

ambayo yanatoshana na asilimia arobaini na nne ya jumla ya mazao yote yanayotumika barani Afrika. Alisema kwamba ili bara la Afrika kuweza kujikomboa kutokana na madeni hayo na kuweza kukabiliana na karne ya 21 bila madeni, lazima liweze kukabiliana na umaskini, njaa, magonjwa na ujinga, vilevile kuwa na viongozi ambao wana nguvu na wanaojiamini, wawe wavumbuzi wa dhana au mawazo makuu.

Viongozi hawa lazima waweze kuwatawala wananchi wake na vilevile wanaoweza kujitolea vilivyo katika maendeleo ya nchi zao. Wawe wanawezesha kuwepo kwa amani na undugu baina ya mataifa. Viongozi hawa kwa upande mwingine lazima kuwahamasisha na kuwahusisha katika utaratibu wa uaminifu, kufanya kazi kwa bidii, kutegemea matunda ya jasho lao ili kuboresha maisha yao. Alizidi kusema kwamba katika historia nchi ambazo hazina viongozi wa aina hii hazina falsafa ya uvumilivu na zimebakia kuwa katika woga wa tishio unaotoka nje. (Tim, 1988:6-7)

## **2.5 Uongozi Barani Afrika**

Enzi za zamani hasa katika Bara la Afrika, kiongozi mzuri alipimwa kulingana na jinsi alivyoundwa mkono na watu wengi, hii ilifanyika kwa njia ya wazi na iliyokubalika pasipo kuuliza, kwa jinsi viongozi walivyojijhusisha na mambo ya watu. Uongozi ulitokana na makubaliano ya wengi na wala sio kwa kulazimisha kama ilivyo sasa. Wakati huu maoni kuhusu kiongozi mzuri ni tofauti na hufafanuliwa kwa kutumia sifa bainifu za jinsi mambo yanavyofanyika na hutegemea ukiritimba wa kulazimisha uhalalishi ili kuweza kuudumisha Sandbrook (1985). Kutokana na mtazamo huu, Amaoko, kama alivyonukuliwa katika Ochola (2007:17) anajadili kwamba, jambo la kwanza la kufanya kuhusiana na taifa ambalo lina lengo la kuhalalisha na kuwa na uongozi mzuri linahitaji kushughulika na kuimarisha maendeleo ya kikatiba na zile kanuni za sheria. Sharti la pili ni kutilia mkazo vijenzi vya

demokrasia ambavyo vingekuza kushiriki kisiasa kwa wananchi wote katika kulikuza taifa lao siku baada ya siku.

Katika Bara la Afrika, pale ambapo watawala wa Kikoloni walikuwa na ushirikiano na watawala wa Kiafrika walizalisha katiba ambayo haikuwa na misingi ya kisiasa katika tamaduni za Kiafrika, bali waliziandika katika karatasi ambapo zilikuwa zitumike tu. Sandbrook (1985) katiba hiyo iliishia kuwa na mataifa ya kinyonge, yanayofeli na yaliyofeli kabisa, yanayojulikana kama ("*3 Fs*" *Fragile, Failing and Failed states*) na vilevile kutoa kumbukumbu ya aina ya serikali zinazopatikana. Hali ya kuwa tofauti baina ya nchi nyingi barani Afrika imeenea mno kwa kuweco kwa historia ya Ukoloni tofauti tofauti, mifano ya uongozi ambayo ilizuka katika kipindi hicho ilizalisha mataifa ambayo yana sifa bainifu ambazo zinaweza kutumiwa kuelezea uongozi mzuri. (Sandbrook, 1958)

Uongozi katika nchi nyingi za Afrika unaonyesha kwamba hubakia kwa wanajamii walewale. Kwa mfano nchini Kenya kulikuwa na maendeleo kwamba uongozi ungerithiwa. Wanajamii walikubaliwa kuchukua ofisi za kisiasa. Himbara (1994), anaonyesha orodha ya mawaziri waliorithi viti vya ubunge wakati jamaa zao walipokufa.

Bila shaka hali hii ya kupokezana uongozi kutoka kwa kiongozi mmoja hadi mwingine wa jamii ile ile utaufanya mfumo wa uongozi kuwa ni ule ule uliotumiwa na mwanajamii aliyetangulia. Aidha mchango wake katika maendeleo ukawa ni ule ule pasipo na kubadili mambo. Ikiwa mabadiliko yalikuwa mazuri huenda yakawa mazuri zaidi na ikiwa yalikuwa mabaya basi yatakuwa mabaya zaidi. Labda ingekuwa mwafaka kuzuia viongozi kurithiwa ili kuondoa matatizo yanayoikumba jamii na wananchi kwa jumla.

Wafrika wengi waliamini kwamba na ni haki kusema uhuru ungekaribisha mwamko mpya kama jitihada za ukombozi kabla hata ya kuweza kujitegemea, uhuru ulileta hisia mpya katika kujifunza kwa minajili ya hamu na matarajio ya wengi. Kwani inaonyesha kwamba kule kupigania uhuru hakukuleta funzo la kutosha kuanzisha mwafrika mpya ambaye angefanya vitu tofauti ili kuwabadilisha wananchi wenzake kwa kuwafaidi, mbali baadhi ya viongozi waliokuwa wameongoza katika kupigania uhuru walikuwa tayari wameshinikizwa na uongozi wa ukoloni na hawakuonyesha tofauti baina yao na wale wakoloni. Tofauti ilikuwa tu baina ya nyuso zile nyeupe na zile nyeusi.

Mseto mpya ulikuwa umebuniwa kati ya uwezo wa wale Wakoloni waliokuwa wanaondoka na tabaka la juu la wale Wafrika waliochukua usukani. Mfumo ule wa uongozi wa kikoloni ulikuwa haujavunjika kama anavyo Oginga Odinga katika *Not yet uhuru* (1968).

## **2.6 Uongozi Katika Afrika ya Mashariki**

Zaidi ya kutazamia mabadiliko ya kisiasa, mataifa mengi barani Afrika na hususan Afrika ya Mashariki yalitarajia mabadiliko katika sehemu nyingine za maisha. Hali ya maisha ilikuwa ikiboreka katika maeneo mengi ya ulimwengu. Maendeleo ya katiba yalituwezesha kufanya mambo ambayo hayangewezekana miaka kadhaa mapema. Uchumi ulistawi haraka katika nchi nyingi hivi kwamba ilitarajiwa kungekuwa na ufanisi ulimwenguni pote . Ilionekana kwamba mambo yako shwari.

Katika karne ya ishirini na moja, miaka kadhaa baadaye tunajiuliza ni nini kilichotokea, inaonekana kwamba mambo yanaenda kinyume na ilivyotarajiwa. Mara nyingi vyombo vya habari huripotivi visa vya ajabu kama mashambulizi ya kigaidi, ufnisadi, ongezeko la silaha za mashambulizi, ubakaji, uporaji wa mali ya umma, na mambo mengine yenye kuhuzunisha. Matukio haya yanazidi kugawanya mataifa na jamii zake. Hii inaonyesha kwamba

tumenaswa katika ulimwengu uliojaa jeuri kwa sababu ya matendo ya watu huku wakiongozwa na viongozi katika kulipiza kisasi.

### **2.6.1 Uongozi Nchini Tanzania**

Nchi ya Tanzania ni mfano wa baadhi za nchi ambazo tumeshuhudia zikibadilika kutoka nchi ambayo ilijitegemea na kuwa taifa ambalo lilitegemea msaada wa kigeni. Viongozi wa serikali baada ya kutoa ahadi waligeuka kuwa waongo. Mfumo wa Ujamaa ulioanzishwa na kiongozi wa nchi hii uliishia kutumiwa vibaya na viongozi. Sehemu hii itatuangazia baadhi ya mifumo ya sera zilizobuniwa na viongozi na hali mbaya iliyojiri na ingalipo hadi wa leo, hali ambayo ilizifanya ndoto za Watanzania kudidimia.

Ujamaa ni siasa iliyoanzishwa kwa misingi ya sera za Julius Nyerere za maendeleo ya kijamii na ya kiuchumi katika Tanzania punde tu baada ya Tanganyika kupata uhuru kutoka Uingereza mwaka 1961. Mwaka 1967 Rais Nyerere alichapisha mwongozo wa maendeleo yake, ambao uliitwa Azimio la Arusha, ambapo alionyesha haja ya kuwa na mtindo wa Kiafrika wa maendeleo, huo ukawa msingi wa usoshalisti wa Afrika. Ujamaa linatokana na neno la Kiswahili linalomaanisha familia au jamii, na hujulikana kwa sifa kadhaa muhimu, yaani mtu anakuwa mtu kwa kupitia watu au jamii.

Nyerere alitumia Ujamaa kama msingi wa mradi wa maendeleo ya taifa. Aliifasiri dhana ya Ujamaa kuwa mfumo wa usimamizi wa kisiasa na wa kiuchumi kwa njia mbalimbali; kuweko kwa mfumo wa chama kimoja chini ya uongozi wa chama cha mapinduzi (CCM) ili kusaidia katika kiumarisha mshikamano wa kujitegemea kwa Tanzania iliyokuwa tu imepata uhuru. Ustawishaji wa usawa kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa kuweko kwa demokrasia kuu; kukomesha ubaguzi kwa misingi ya hali ya mtu; na kuzifanya sekta muhimu za uchumi



kufikia taifa zima,(Pratt 1999:137-139). Kupeleleza uzalishaji katika vijiji, ambapo ilifanya uwezo wa uzalishaji wa aina zote kufanyika kwa pamoja. Kukuza kujitegemea kwa Tanzania kwa njia mbili: Mabadiliko ya kiuchumi na mitazamo ya kiutamaduni. Kiuchumi, kila mtu angekifanyia kikundi chote kazi na kujifanyia yeye mwenyewe, kiutamaduni ni lazima watanzania wajifunze kujikomboa kutoka kwa utegemezi wa nchi za Ulaya. Kwake Nyerere, ilijumuisha Watanzania kujifunza kujifanyia mambo wao wenyewe na kujifunza kuridhika na kile ambacho wangeweza kufikia kama nchi huru. Utekelezaji wa elimu bila malipo na ya lazima kwa Watanzania wote ili kuwahamasisha wananchi kuhusu kanuni za ujamaa.

Uongozi wa Julius Nyerere ulivutia Tanzania, macho na heshima ya kimataifa kutokana na msisitizo wake wa maadili kama msingi wa maamuzi ya siasa. Chini ya Nyerere Tanzania ilipiga hatua kubwa katika vipengele vya maendeleo; vifo vya watoto vilipungua kutoka 138 kwa 1000 waliozaliwa hai mwaka 1965 hadi 110 mwaka 1985; tarajio la kuishi lilipanda kutoka 37 (1960) hadi 52 (1984); uandikishaji wa wanafunzi katika shule ya msingi ulipanda kutoka 25% (16% tu kwa watoto wa kike) mwaka 1985 (ingawa idadi ya wananchi ilikuwa inaongezeka kwa kasi); asilimia ya watu wazima waliojuwa kusoma na kuandika ilipanda kutoka 17% mwaka wa 1960 hadi 63% mwaka 1975 (juu sana kuliko nchi nyingi za Afrika) ikaendelea kupanda.( Colin 1995 )

Plaut (2012), hata hivyo Ujamaa (kama vile mipango mingine ya uzalishi wa pamoja) ulipunguza uzalishaji hata kutia shaka juu ya uwezo wake wa kustawisha uchumi. Hatimaye sababu mbalimbali zilifanya Ujamaa uonekane umeshindikana kiuchumi. Kati ya hizo, tatizo la Kimataifa la mafuta ya 1970, anguko la bei ya bidhaa zilizozalisha nchini (hasa kahawa na katani), utovu wa uwekezaji kutoka nje ya nchi na vita vya Uganda–Tanzania miaka 1978-1979 vilivyofyonza sana mtaji muhimu na miaka miwili mfululizo ya ukame.

Kufikia mwaka 1985 ilikuwa wazi kwamba Ujamaa ulishindwa kutoa Tanzania nje ya ufukara wake; Nyerere alitangaza kuwa atang'atuka asigombe tena urais katika uchaguzi wa mwaka huohuo. Ujamaa ulivunjwa (ingawa si kinadharia) mwaka 1985 wakati Nyerere alipomwachia Ali Hassan Mwinyi aliyeingiza nchi katika taratibu za soko huria, (O'conner 2004). Nyerere alitumia sheria ya kuzuia kutiwa nguvuni bila sababu, kukandamiza vyama vya wafanya kazi na kuwakamata wapinzani kikatili kupindukia, walioadhiriwa huhesabiwa kuwa maelfu. Mashirika ya kimataifa ya kutetea haki za binadamu kama Amnesty International yalipiga kampeni dhidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu Tanzania. (Colin 1995)

Vyombo vya habari nchini vilidhibitiwa kwa kunyimwa usajili rasmi, serikali iliwalizimisha watu kuhamia mashamba ya pamoja, jambo ambalo lilitatiza shughuli za kilimo na uzalishaji. Watu walipoteza heshima kwa utamaduni na maeneo kama vile makaburi ya mababu zao. Polisi na wanajeshi waliojihami kwa silaha walitumika katika uhamisho wa watu. Tanzania iligeuka kutoka taifa la wakulima waliojitahidi kukidhi mahitaji yao na kuwa taifa la wakulima walioangamia kwa njaa kwa pamoja. Taifa lilinusurika kwa kutegemea msaada wa kigeni wa chakula ambacho kilipewa tu watu waliokubali kujiunga na Ujamaa. (Porter 2006)

Serikali ya Tanzania iliwapa ahadi ambazo baadaye ziligeuka kuwa uwongo. Uchumi ulianguka na kiasi kikubwa cha utajiri wa nchi ya mijengo na kuboresha miundo ya ardhi (mashamba, miti ya matunda,) iliharibiwa au kutelekezwa kwa lazima. Suleman Sumra aligundua kuwa mavuno katika mashamba ya Ujamaa kwa pamoja yalikuwa chini kwa asilimia 33-85 kuliko yale ya mashamba yaliyomilikiwa kibinafsi. Kwa wastani yalikuwa chini kwa asilimia 60. Wakulima wa pamoja hawakuwa na motisha wa kufanya kazi. (Porter 2006)

Hali ya nchi ilienea haraka na kuathiri karibu kila sekta. Mwaka 1967, ustawishaji wa taifa ulibadilisha serikali na kuifanya mwajiri mkubwa zaidi katika nchi. Ilihusika katika kila kitu, kuanzia kufanya mauzo ya rejareja hadi biashara ya kuuza na kuagiza bidhaa kutoka ng'ambo na hata uokaji, na kuleta mazingira muafaka kwa ufisadi.

Ukiritimba na taratibu zisizoeleweka ziliongezeka na viwango vya juu vya kodi kuwekwa. Fedha za umma zilitumika vibaya na kuweka kwa matumizi yasiyo na faida. Uwezo wa kununua ulipungua kwa kiwango kikubwa mno na hata bidhaa muhimu zikawa hazipatikani. Mfumo wa kutoa vibali uliwaruhusu maafisa wakuu kuchukua rushwa kubwa ili kutoa vibali. Msingi wa mfumo wa ufisadi ukawa umewekwa. (Stapenhurst, 1999:153-156)

Thomas (1991:24), Barabara ziliharibika na kuwa kati ya barabara mbovu zaidi barani Afrika. Sekta ya viwanda ikadidimia. Kampuni ya mgodi iliyomilikiwa na serikali ikaonekana kushindwa. Benki ya Dunia pia imekosolewa kwa kuchangia mpango huo. Nchini Tanzania, kwa mfano, Benki hii ilitoa fedha kwa kampeni ya udikteta wa Julius Nyerere unaoitwa Ujamaa, ni mfano wa mfumo wa vijiji wa Mengistu. Wakulima walipoteza uhuru wao, na nchi ilichukua ardhi yao na kudai mauzo yao, yote haya kwa msaada na baraka za Benki ya Dunia. Katika miaka michache tu, Nyerere aligeuza nchi yake kuwa gofu, taifa la waombaji. Lakini Benki hii haijawahi kukubali makosa hayo. (Yonas, 1988)

Muziki wa hip hop nchini Tanzania ulipata msukumo kutokana na mawazo na mandhari ya Ujamaa. Mwaka 1967, baada ya Rais Nyerere kuanzisha itikadi mpya ya siasa, ambayo aliahidi itawakomboa Watanzania kutoka ubeberu wa kimataifa, ilitelekezwa na wanasiasa wa Tanzania, kanuni za Ujamaa zilifufuliwa tena kupitia njia isiyotarajiwa:

Wanamuziki wa *Rap* na wasanii wa *Hip Hop* katika mitaa ya Tanzania.(Sidney, 2011:230-254)

Denied (1967:73), Kama jawabu kwa miaka ya viongozi wafisadi wa serikali na wanasiasa baada ya Nyerere, dhana za umoja na familia na usawa zilikuwa ndio ujumbe uliotumwa katika muziki uliokuwa unatayarishwa. Hii ilikuwa kama mwitikio wa darasa la wafanyakazi katika mtazamo fulani ilikuwa upinzani. Kanuni za uchumi wa ushirika "wananchi wa kawaida kushirikiana ili kujipatia mahitaji muhimu ya maisha" ni maneno yanayoweza kuonekana katika nyimbo nyingi za *Hip Hop* za wasanii wa Tanzania. Zinapigia upatu ukuzaji wa biashara na kujitegemea katika jitihada za kuinua mioyo ya vijana na kuhamasisha mabadiliko katika jamii.

### **2.6.2 Uongozi Nchini Kenya**

Kumekuwa na dhana tofauti kuhusu wazo la Afrikanaizesheni na kusalia kuwa swala lisiloeleweka vizuri. Kumetokea shida za kuweza kuifafanua sio tu kuhusu wazo lenyewe lakini pia kutambua linahusu nini au kuashiria nini.

Afrikanaizesheni haihusu kuwaondoa Wazungu na utamaduni wao, lakini inahusu kuthibitisha utamaduni wa Kiafrika na utambulisho wao katika jamii ya dunia. Sio mfumo wa kuondoa, lakini ni mfumo wa pamoja. Ni wa masomo na njia za maisha kwa Waafrika. Inahusu kushirikisha, kurekebisha na kuingiza tamaduni zingine ndani na kupitia maono ya Kiafrika ili kuleta uwezo au nguvu, mageuko na mabadiliko ya urahisi yaliyo muhimu ulimwenguni. Afrikanaizesheni ni mfumo wa kufafanulia au kuelezea utambulisho wa Kiafrika na utamaduni wake. (Makgoba, 1997:199)

Afrikaizesheni hushikilia kwamba ujuzi wa Kiafrika ndio kwa ujumla msingi na vianzo vya ujenzi wa aina yoyote ya elimu. Vilevile ni utetezi wa haki unaofahamika ambao ni wa kimaksudi unaoonyesha haki za kuwa Mwafrika (Ramose, 1998).

Mnamo mwaka wa 1967 miaka michache baada ya uhuru, nchi ya Kenya ilibuni sera katika mkataba wa Kenyaizesheni au Afrikaizesheni ili kuufaulisha mkataba wenyewe. Baadhi ya sera ziliwadhuru wale ambao hawakuwa raia wa Kenya baada ya uhuru. Sera katika mkataba huo zilidai kwamba wale ambao hawakuwa raia wa Kenya wangeendesha biashara zao katika maeneo makhususi na vilevile hawakushiriki katika kuzalisha bidhaa zilizotumiwa nchini.

Katika Rotchild (1969:689), sera zilizobuniwa zilihitiwa kuwepo kwa mikakati maalum katika jinsi ya kuwachagua na kuwateua wananchi watakaofanya kazi katika mashirika ya umma na njia makhususi za ugavi wa rasimali kwa usawa bila mapendeleo. Sera hizo zingetatua ubishi uliokuwepo kuhusu usawa na maendeleo ya uchumi kati ya waliobahatika na wale wasiobahatika, kati ya Waafrika na wale ambao hawakuwa Waafrika.

Kwa upande mwingine sera zilihitiwa serikali iweze kutosheleza mahitaji halali kwa fursa za Waafrika kwa sababu wale ambao hawakuwa Waafrika (Wazungu na Wahindi) ingawa walikuwa wachache ndio walimiliki nyadhifa muhimu serikalini na hata katika mashirika ya kibinafsi.

Serikali ilitilia mkazo mfumo wa Afrikaizesheni kama sera za kuwaandikisha waafrika wengi katika nyadhifa hizo kwa kutoa elimu na ujuzi uliostahili. Kwa sababu wananchi wengi sasa walikuwa wanapata elimu na ujuzi wa kutosha, serikali ilihitajika kupanua soko la

makazi kwa kujenga viwanda vingi katika sehemu zilizokuwa na uhaba wa maendeleo ili kutosheleza mahitaji ya wananchi. (Rotchild, 1969:690)

Hata baada ya sera hizi kubuniwa Kenya bado inashuhudia kutolingana kwa jamii na vilevile kutolingana kwa makabila katika nyadhifa tofauti tofauti. Kutolingana kwa nafasi kati ya makundi ya kijamii kumebakia kuwa jambo sumbufu katika maisha nchini Kenya leo hii. Hata ingawa tunaweza kuuhusisha na sababu zilizoridhiwa kabla ya uhuru kama kwa mfano; kuwa na shule za matabaka, nyumba na hali za matibabu kuwa vya viwango tofauti kulingana na uwezo wa watu tofauti, kutokuwa sawa huku kunasabisha mivutano ya kisiasa na kuonekana waziwazi.

Hata kama serikali ya Kenya ilifutilia mbali mambo ya matabaka kama shule za Kimbari, nyumba na hospitali za Kimbari, inadhihirika kwamba athari zake bado zingalipo na zinashuhudiwa hata katika uchumi wa nchi.

Viongozi serikalini walilazimika kubadilisha mambo yaliyopewa kipaumbele kati ya usawa na maendeleo nchini na hata vilevile katika madai ya makundi. Kwa sababu muachano wa kijamii huhusisha mgawanyiko mkubwa, mahitaji ya wale Waafrika walio wengi kupata usikivu mwangalifu na wenye huruma kutoka kwa viongozi wa kisiasa. Lakini pale uzoefu wa usawa na hamu ya kupata huleta hisi ya mshikamano kwa upande wa jamii ya Waafrika, mipaka ya baina ya makabila hupunguzwa na mahitaji kwa usawa huchanganywa na malengo ya maendeleo.

Kwa sababu hii palizuka makundi mawili yaliyopishana. Kundi la kabila la wale wachache ambapo jamii ya Waafrika ilikuwa kubwa, katika kundi la pili Wazungu, Wahindi na Waafrika wachache. Makundi haya yalikuwa na mahitaji tofauti na malengo tofauti, kwa

hivyo mahitaji yao kwa serkali ilikuwa tofauti. Mara nyingi serikali na viongozi hulazimika kutilia maanani mahitaji ya walio na udhaifu huku ikilazimika kupunguza ukuaji wa maendeleo. Lakini hii hutumiwa kama kipimo cha uongozi unofaulu katika mataifa yanayoendelea kama Kenya. Huenda ikawa ndiyo sababu moja ya maendeleo nchini kutatizwa na kurudi nyuma.

### **2.6.3 Uongozi Nchini Uganda**

Mara tu baada ya Uganda kujinyakulia uhuru mwaka wa 1962 wanachama waakilishi wa chama cha Uganda People's Congress, walikusanyika tarehe ishirini na nne, mwezi wa kumi mwaka wa 1969, katika mkutano wa dharura mjini Kampala. Wao ndio waliokuwa na jukumu la kubuni sera ambazo zingetumika katika kuiongozo nchi yao. Mkataba uliobuniwa ulijulikana kwa jina la "*The Common Man's Charter*" ulinuiwa kutoa utambuzi wa maana halisi ya uhuru, kwamba maliasili ya nchi, mali na sanaa zitumike kwa faida ya watu wote wa Uganda kwa makubaliano ya kanuni za ujamaa.

Mkataba huo ulionyesha jinsi Waakilishi wa chama chao wangejitolea kuanzisha mapatano ya usalama wa kutosha, haki, usawa, uhuru wa kujiamulia na ustawi wa vijana wa Taifa la Uganda. Na kwa kuweza kuafikia malengo hayo walihusisha mbinu za mikakati ya kuelekea kushoto kama misingi ya utaratibu huo. Kuelekea kushoto kulihusu ubunifu wa utamaduni mpya wa Kisiasa na njia mpya ya maisha, pale ambapo wananchi wa Uganda kwa jumla, maslahi yao na sauti zao katika serikali ya Taifa na vilevile katika mamlaka za mashinani ilikuwa muhimu zaidi. Na kwa hivyo sio za kikabila na sio za Kibepari.

Mkataba uliobuniwa ulihakikisha kwamba Uganda nzima ingehusisha wananchi wote katika maendeleo yake, na hakuna mtu yeyote yule angefaidika kwa kuwatumia wenzake. Ulinzi

ungetolewa kwa usawa, ugavi wa mali na rasilmali ungesawazishwa bila mapendeleo au ukabila kwa misingi ya Kimbari, rangi, dini au tabaka. Wananchi wote walistahili kufurahia matunda ya uhuru kwa usawa bila ubaguzi.

October 9, 1962 ndio hasa ulikuwa mwanzo wa mivutano mikubwa ya aina tofauti katika barabara ya kuelekea kupata uhuru kamili kwa hivyo tarehe hii kwa mtazamo wa chama cha U.P.C hakukuwa mwisho wa kupata uhuru bali ulikuwa mwanzo wa kujenga nchi.

Lakini chini ya miaka kumi baada ya uhuru ndoto za kumwendeleza Mwafrika zilianza kudidimia. Masuala makuu na ya kutisha kuhusu siasa yaliyowakumba wananchi wa Uganda hayakuwa hasa sababu za wananchi wenyewe kuhusika. Masuala hayo nyeti yalisababishwa na umbo la serikali kuhusu Uganda iliyokuwa huru na nani angestahili kuwa rais wa Taifa kwa minajili ya kufanikisha uhuru. Suala hili ndilo lililochukuliwa kuwa muhimu zaidi, na sio kwamba suluhu ingepatikana ikiwa wangezingatia maslahi ya mwananchi. Lakini kwa sababu makabaila, kwa kusingizia maslahi ya wananchi waliona uhuru kama tishio kwa nyadhifa walizoshikilia. Waliomba kufanya nyadhifa hizo kuwa zenye mahitaji sawa na yale yaliyokuwepo ili waendeele kuzishikilia na kutawala kama walivyotawala hata kabla ya uhuru. Walitaka kuwanyima wananchi fursa ya kuchangia katika kupalilia uhuru.

Uganda wakati huu iko katika hatari ya kuwa sikitiko jingine la Africa, linaelekea kufeli kwa sababu ya kujenga upya serikali na uchumi wake chini ya viongozi ambao walisahau sera zilizobuniwa na mkataba wa *Common Man's Charter*. Kwamba kwao mwananchi hahusishwi katika uchumi wa nchi. Viongozi hawa shupavu wanahatarisha kufuja au kuharibu hiba ya nchi yake. (Woodrow, 2005)



Kwa mfano historia ya chama cha NRM katika nchi hii kinatambuliwa vizuri. Kilichukua uongozi mnamo Januari Mwaka 1986. Kiliandikisha rekodi ya kurudisha miaka kumi ya kwanza uongozini. Kilikuwa na malengo matatu ambayo chama hiki kilistahili kuhitimisha. Kwanza kiliimarisha serikali yenye nguvu katika maeneo yote ya nchi isipokuwa tu maeneo machache ya Kusini. Pili kiliboresha uchumi kwa usaidizi wa wafadhili wa kimataifa. Jambo la tatu NRM ilianzisha na ambalo haikukamilisha ni kubuni asasi ambazo zingewajumuisha wananchi wa maeneo yote na kutoa suluhu za tofauti zao chini ya sheria za Kidemokrasia. Jambo ambalo lilihimizwa na mkataba wa C.M.C kushindwa kutekeleza lengo hili la tatu ndipo sasa nchi iko hatarani. (Woodrow, 2005)

Uongozi wake umefika katika enzi ambayo mamlaka huishia katika mchanganyiko wa ufisadi, uungwaji mkono na kujiendeleza kupitia utawala wa hila wa mageuzi kutoka mfumo wa uongozi wa chama kimoja hadi mfumo wa vyama vingi.

## **2.7 Hitimisho**

Katika sura hii tumevipitia vigezo muhimu na vya kimsingi kwa kazi hii. Kazi hii imechunguza dhana ya uongozi na kutoa mifumo tofauti ya uongozi ili kuweza kufikia uamuzi wa kiongozi mzuri au kiongozi mbaya. Vilevile tumetaja baadhi ya changamoto zinazowakumba viongozi katika uongozi wao na kuwalazimu kuchangia katika mabadiliko mbalimbali ya jamii zao.

Tumeangazia uongozi barani Afrika hususan Afrika ya Mashariki pamoja na viongozi wake na mifumo wanayotumia kwa kina kwa sababu ni muhimu katika kazi hii ili kupata ufahamu wa mchango wao katika mabadiliko ya nchi zao. Tumeangalia kwa kifupi baadhi ya sababu zinazopelekea mabadiliko hayo na athari zake. Hivi ni vigezo muhimu katika utafiti huu kwa sababu ndivyo mihimili ya utafiti wetu.

## SURA YA TATU

### UCHAMBUZI WA MAUDHUI NA WAHUSIKA KATIKA VIPANYA VYA MAABARA

#### 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili, tuliangazia viongozi pamoja na uongozi barani Afrika hususan Afrika ya mashariki na mifumo wanayotumia. Tuliona jinsi walivyosababisha mabadiliko katika nchi zao kwa kutumia uwezo na mamlaka waliyo nayo. Tumeangalia kwa kifupi baadhi ya sababu zinazopelekea mabadiliko hayo na athari zake. Yote haya, kimsingi ni kwa sababu viongozi huamini kwamba wao tu ndio wana uwezo wa kuleta mabadiliko pasipo kujumuisha jamii. Yaani wao ndio wana uwezo wa kudhibiti usemi hivyo basi lolote wasemalo au wafanyalo halipingiki. Kwamba kadri wanavyopata uwezo na fursa ya semi tofauti tofauti, ndivyo wanavyoweza kutwaa uwezo mkubwa, Van Dijk (2001).

Katika sura hii tumechunguza na kuchanganua aina tofauti tofauti ya viongozi wanaopatikana katika riwaya ya *Vipanya vya Maabara* (2007). Baadhi ya mambo ambayo tumeangazia ni pamoja na aina ya viongozi huku tukiwalinganisha na viongozi wetu wa hali halisi, maudhui katika riwaya hii kwa mfano ufisadi, dhuluma, ubakaji miongoni mwa mengine katika makundi mbalimbali ya vipanya vya maabara pamoja na changamoto ambazo makundi hayo yanazipitia. Aidha tumeonyesha jinsi viongozi wa riwaya hii wanavyosababisha mabadiliko kwa kutumia mkakati wa kudhihirisha nguvu za usemi na vilevile mkakati wa ubishi katika jamii yake na matokeo yake.

### **3.1 Muhtasari wa Vipanya Vya Maabara**

*Vipanya Vya Maabara* ni riwaya yenye mvuto mkubwa unaotokana na hadithi ya kuisimua juu ya Bob Kerogo, ambaye ni mhusika mkuu, jamaa zake na marafiki ambao ni vijana wa rika lake; Okach, Kamash, Wairi, Gaceri, Swaleh na wengineo. Kwa kutumia tashtiti kulenga wahusika na jamii, tunapata maudhui kama vile ubaguzi, ubakaji, ubinafsi, uufisadi na maovu mengine ambayo jamii ya *Vipanya Vya Maabara* inapitia.

Mbinu nyingine za uwasilishaji kama vile taharuki, mbinu rejeshi na mshtukizo zimetumiwa ili kusimulia jinsi Bob anavyokulia katika mazingira yenye matatizo chungu nzima katika eneo wanamoishi walalaho huko Parklands na vitongoji vingine jijini Nairobi. Bob anayakabili maisha kwa ujasiri na matumaini huku akifanya kazi za sulubu kama vile kuajiriwa katika maeneo ya viwandani na kuosha magari jijini nje ya *Safari Hotel*. Pia anaajiriwa kama dereva na Vera, mwanamke aliye na asili ya kizungu ambaye hatimaye anakuwa kipenzi chake.

Bob anachapa kazi hizi bila kulegea wala kukata tamaa. Hatimaye maisha yake yanabadilika ghafla anapofichua siri ya mauaji ya Rita King, bintiye Seneta Humphrey King wa Marekani. Kifo cha Rita kinasababishwa na waziri Rashid Hamisi. Bob anapofichua siri hii, anakabidhiwa zawadi ya dola milioni moja. Analala maskini na kuamka tajiri. Jambo la kusikitisha ni kwamba marafiki wa Bob ambao ni wa rika lake wanafariki kwa njia tofauti zinazosababishwa na nyendo mbaya pamoja na utovu wa nidhamu na maadili. Baadhi ya nyendo hizo ni pamoja na ujambazi, matumizi ya mihadarati, uufisadi, ugonjwa wa ukimwi, malezi mabaya miongoni mwa mengine.

Hii ni riwaya ya Kisosholojia au Kijamii ambayo inasawiri maisha ya kawaida ya jamii. Katika kusawiri maisha, riwaya hii inaeleza matatizo hayo ambayo kwa mujibu wa jalada, Vipanya Vya Maabara ni fumbo ambalo linaashiria mambo kadhaa kama vile, mfumo uliopo wa elimu, uongozi, utabaka ambao unatumika na watawala kufanyia utafiti watawaliwa. Neno vipanya limetumiwa kijazanda kurejelea makundi mbalimbali ya watu katika maabara kwa mfano, makundi ya vijana wanaotumiwa na wanasiasa (viongozi) kutekeleza uhalifu kama kuuza mihadarati, ujambazi, ukahaba na maovu mengine.

Dhamira kuu katika riwaya hii ni kuangazia maisha ya jamii katika muktadha wa hali ngumu kiuchumi na kisiasa katika miaka ya themanini na tisini. Huu ni wakati ambapo taifa la Kenya lilisakamwa na ufukara, ufidiaji, uozo wa kimaadili na kuporomoka kwa asasi za kielimu, kiafya na kiuchumi jambo ambalo bila shaka lilichangiwa pakubwa na viongozi wa nchi hii.

### **3.2 Tathmini Ya Maudhui Kuhusu Makundi Ya Vipanya Vya Maabara**

Maudhui ni yale yaliyomo au jumla ya masuala yanayozungumziwa katika kazi ya Kifasihi yoyote. Maudhui huibuka katika uendelezaji na ukuzaji wa dhamira ya kazi fulani. Njogu na Chimera (2011:93) wanaeleza maudhui kama mawazo ya mtunzi kwa mkabala na muktadha fulani. Yaani ni Masuala makuu ya utungo dhamira, lengo, shabaha yanapounganishwa na muktadha wa utungo. Naye Wamitila (2008) anaeleza maudhui kama jumla ya mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya fasihi. Aidha maudhui huweza kueleza kinachoshughulikiwa.

Katika sura hii maudhui ndiyo yalituelekeza kutambua makundi ya vipanya katika riwaya hii na kutupa fursa ya kujibu swali la “nini” riwaya hii ilizungumzia ambapo tuliweza kuorodhesha njia tofauti zilizotumiwa na viongozi katika kuleta mabadiliko katika *Vipanya Vya Maabara*.

Tulitanguliza kwenye Sinopsia kueleza kwamba *Vipanya Vya Maabara* ni riwaya ya kisosholojia au kijamii katika kusawiri maisha, riwaya hii inaeleza matatizo hayo ambayo kwa mujibu wa jalada, *Vipanya Vya Maabara* ni mfumo uliopo wa elimu, uongozi, utabaka ambao unatumia na watawala kufanyia utafiti watawaliwa. Neno hilo vipanya limetumiwa kijazanda kurejelea makundi mbalimbali ya watu katika maabara.

Katika hali halisi, vipanya vya maabara ni aina ya panya maalumu wanaofugwa katika maabara kwa lengo la kufanyia utafiti wa majaribio ya tiba sababu kuu ya kuwatumia panya hawa ni kwamba mfumo wa maumbile yao huwa kama ya binadamu na huweza kutoa matokeo mazuri. Vipanya kama hivyo, hupewa kemikali au dawa inayofanyiwa utafiti ili kukadiria ufanisi wake au hata athari zake. Wanasayansi wanapofanya utafiti wao hawajali kamwe kuhusu maisha ya vipanya hivyo. Lengo lao muhimu ni kudhibitisha ikiwa wanayoyadadisi ni kweli na baada ya jaribio fulani na matokeo kuandikishwa vipanya hivyo huangamizwa maksudi na wanasayansi hao. Jinsi wanasayansi wanavyoangamiza vipanya hivyo, ndivyo vilevile viongozi katika *Vipanya Vya Maabara* wanavyoangamiza jamii yake.

Makundi ya vipanya katika riwaya hii ni pamoja na mfumo wa elimu wa 8-4-4 ambao serikali inatumia kufanyia utafiti katika taasisi za elimu, makundi ya vijana wanaotumiwa na wanasiasa kutekeleza majukumu yao, watawaliwa wanaotumiwa na watawala kufanyia utafiti wao, afisa wa polisi wanatumia njia tofauti kujinifaisha kama vile ufisadi, ukahaba, wizi wa

kimabavu, mataifa yaliyoendelea wanatumia mataifa yanayoendelea katika tafiti zao, tabaka la juu linatumia tabaka la chini kufanya utafiti wake baina ya makundi mengine.

Sababu kuu ya kuchunguza makundi haya katika utafiti huu ni kwamba, viongozi mbalimbali ndio haswa wanaojishughulisha na tafiti hizi na katika hali ya kuendeleza utafiti wao, wanyonge wanaadhirika kiafya na hata uchumi wa nchi nao unaathirika vilevile maadili ya kijamii yanavurugwa.

### **3.2.1 Mfumo wa Elimu wa 8-4-4**

Huu ni mfumo wa elimu ulioanzishwa mwaka wa 1985 nchini Kenya. Viongozi wa nchi ya Kenya chini ya rais wake waliuanzisha mfumo huu uliochukua miaka minane katika shule za msingi, miaka minne katika shule za upili na miaka minne ya chuo kikuu. Tangu mwaka huo hadi sasa elimu ya umma nchini Kenya imejikita katika mfumo huo. Mfumo huu nia yake haswa ilikuwa kuweza kuwatayarisha wanafunzi ili baada ya masomo yao waweze kujitegemea. Kweli nia ya mfumo huu ni nzuri pengine utekelezaji wake ungeboreshwa zaidi.

Mfumo huu wa elimu umefanyiwa majaribio mengi ya haraharaka na viongozi wa nchi, majaribio ambayo yamezidisha utata badala ya kuuboresha. Ilisemekana kwamba mfumo huu wa 8-4-4 ulihimiza stadi katika aina mbalimbali za utendaji na ufundi. Uliidhamiria kuwafanya wahitimu wote kuweza kufanya kazi na kujitegemea baada ya kumaliza shule. Mfumo huu ulikuwa mkakati wa kusuluhishia tatizo la ukosefu wa kazi. Ulihimiza sana kazi za mikono ambazo zilichukiwa na kupendelea zile za ofisini. Ungezalisha kazi na hivyo kuharakisha maendeleo. Sifa zake zilienea kote. Lakini hayo yote yameishia kuwa tu majaribio ambayo hayajafaulu. Mfumo huu umepelekea wahitimu kuwa kundi la vipanya wa

kufanyiwa majaribio huku wakiingizwa katika umaskini na ufukara.Mwalimu Keruja anasikika akilalamika,

ovyo kabisa mambo yanavyofanywa katika nchi hii iliyolaaniwa.Kila kitu kinafanywa kama kwamba kuna dharura.Haya mambo ya 8-4-4 yangepangwa vizuri.Shule zipewe muda wa kujenga karakana, maabara na zinunue vifaa vya kutosha.( uk 64)

Maneno kama haya yanayotoka vinywani vya walimu ambao wameaminiwa na wanafunzi wao bila shaka ni ya kuhuzunisha. Ikiwa walimu hawana imani na mfumo huo basi wanafunzi ambao ndio waathiriwa hawataithamini elimu yao na hapo ndipo mwanzo wa matatizo yanazozikumba jamii za *Vipanya Vya Maabara* zinaanzia.

Wanasiasa ambao ndio viongozi wanaohusika na mipango ya elimu nchini, kwa hakika hawajatilia jambo hili maanani.Itawezekanaje aliyehitimu kuwa fundi stadi baada ya masomo yake ikiwa anapomaliza darasa la nane au hata kidato cha nne anachosikia tu ni vifaa kama vile randa na kekee vikitajwa, na pengine kuviona katika vitabu kwa sababu shule haziwezi kuvinunua.Eti sasa akitoka shule atakwenda kujitegemea na kuwa seremala au fundi wa ujenzi.Haya kwa kweli hayawezekani.

Viongozi hawa hujitia hamnazo kuhusu mfumo huu kwa sababu wengi wao watoto wao husomea mataifa ya magharibi ambapo elimu imeboreshwa na wanapohitimu wao hurejea nchini ili kuchukua kazi zote zilizo maarufu.Wananchi huendelea kuumia kwa sababu ya

makosa yanayofanywa na wale wanaodai kuiendesha nchi. Athari za makosa yao haziwafikii kwa sababu wamejitajirisha kwa kutumia nyadhifa zao.

### **3.2.2 Vijana kama kundi la vipanya vya maabara**

Katika jamii nyingi au hata taifa, kwa jumla vijana huchukua asilimia kubwa. Hiki ndicho kiwango muhimu sana maishani mwa binadamu kwani hapo ndipo maisha ya baadaye huumbika au kuumbuliwa. Ni kweli wasemavyo viongozi wengi kwamba vijana ndio viongozi wa kesho lakini jambo hili mara nyingi hua halitimii na hata likitimia hua wamechelewa kwani hawapewi fursa ya kuiongoza taifa au hata jamii.

Katika riwaya hii kuna makundi ya vijana ambayo yanatumiwa na viongozi kutekeleza majukumu yao kama jinzi tuonavyo wanasisia katika hali halisi wakiwatumia vijana wetu katika tafiti zao. Kwa mfano wakati wa uchaguzi, vijana ndio hutumiwa katika kueneza sifa za viongozi na hata kuanzisha vurugu na rabsha.

Waziri wa ulinzi Rashidi Hamisi anawatumia vijana Swaleh, Bob na hata Wairimu katika tafiti zake za ufidia. Anatumia Swaleh kama wakala wake wa kusambaza mihadarati anayouza kwa kiwango kidogo cha fidia bila hata kujali kwamba anahatarisha maisha ya Swaleh na vilevile kudhuru afya ya wanaotumia mihadarati. Waziri Rashidi hana haya kumtumia Bob ili ampate Wairimu na kuweza kupunguza ashiki yake huku akieneza usherati na kuhatarisha maisha ya Wairimu kwa kumuambukiza gonjwa la ukimwi.

Kuna vijana vilevile wanaotumiwa na ofisa wa polisi katika wizi wa kimabavu kwa kuwakodishia bunduki. Wanapowapora watu mali yao, huilipia bunduki ile na pia kuwagawia polisi mali waliyoiba huku wakihatarisha maisha yao na hata vijana hawa huelekea kuuawa



kama ilivyomtendelea Swale pale alipotumia nguvu kuiba kisha akauawa na wale wale polisi waliomkodishia bunduki aliyoitumia kutekeleza uhalifu.

Wazazi wengi wa riwaya hii wamewatumia watoto wao kama makundi ya vipanya kwa kuwatelekeza. Wamepuuzilia mbali majukumu yao huku wakitoa mifano mibaya ya kushiriki katika usherati na ukahaba jambo ambalo limeigwa na watoto wao kwa kuliona kama jambo la kawaida mwishowe linawaangamiza.

### **3.2.3 Tabaka la chini kama kundi la vipanya vya maabara**

Katika hali ya kawaida ya maisha sio muhali kuwaona watu wa tabaka la juu wakiwanyang'anya wale wa tabaka la chini. Ni jambo linaloshuhudiwa hata katika jamii kwamba wale wa tabaka la juu huweza kutambuliwa na huwa na uwezo mkubwa wa kudumisha ubaguzi, uonevu, ukandamizwaji kupitia mikakati tofauti tofauti ya ubishi.

Katika kazi hii tunashuhudia njia tofauti tofauti zinazotumiwa na watu wa tabaka la juu katika kuendeleza ubaguzi na uonevu dhidi ya wale wa tabaka la chini kwa matumizi ya mkakati wa ubishi. Viongozi na watu wa tabaka la juu wanaendeleza ubishi huo kupitia ubaguzi, uonevu, na hata ukandamizwaji. Kwa mfano babake Bob Konstebo Kerogo anabaguliwa na viongozi wa idara ya polisi kwa sababu ya uaminifu na uwazi wake. Viongozi wanamnyima haki yake ya kupandishwa cheo huku wale wanaokuja nyuma yake wanapandishwa cheo na kumuacha palepale. Polisi wengi ambao konstebo Kerogo aliwafunza kazi sasa ni wakubwa wake, akina inspekta Igweta, Okoth, Swaleh na wengine wengi.

Wakubwa wake Kerogo wanamtumia kisha wanamuangamiza hali ambayo inamtamausha konstebo Kerogo hadi anafariki. Waziri Rashid ni kiongozi mwingine ambaye amewatumia

wanyonge wa tabaka la chini katika tafiti zake. Amemtumia Swaleh kama wakala wake kujinufaisha kiuchumi kwa kumuuzia dawa za kulevya huku akiathiri afya ya jamii kwa jumla.

Familia ya Kerogo inabaguliwa na ile ya mjomba wao Mbaabu kwa vile tabaka lao ni la chini. Bob na Freda wanapomtembelea mjomba wao, ni sharti mlinzi wa mlangoni kuuliza ruhusa kutoka kwa mjomba wao ikiwa waruhisiwe kuingia kwake. Lakini maisha ya Bob na mamake yanapobadilika kwa kulala maskini na kuamka tajiri, mkabala wa mjomba Mbaabu na familia yake unageuka na kuwa tofauti kwake Bob na familia yake. Badala ya sasa kuhusiana kama mkubwa na mdogo, mfadhili na mhitaji, sasa walihusiana katika misingi ya usawa na heshima.

### **3.2.4 Ubaguzi wa Kikabila kama kundi la vipanya**

Katika sura ya pili tulishuhudia jinsi uongozi unavyomilikiwa hasa katika Afrika ya mashariki. Viongozi wengi wamelishikilia swala la ukabila na kusababisha maendeleo kurudi nyuma kudai kwamba nchi ni taifa moja na wakati huo huo kulipendelea waziwazi kabila moja, huzidisha mivutano ya kikabila na hivyo kuhakikisha kwamba umoja wa kitaifa haumei mizizi. Mara nyingi watu hulalamika sana kuhusu hali hii, mashirika ya makanisa hujaribu sana kulipinga jambo hili, hata vyombo vya habari hugusia mambo ya ukabila huku vyama vya upinzani vikipaza sauti kupinga ukabila, ingawa navyo huelekea kuwa vya kikabila lakini hakuna kinachobadilika.

Konstebo Kerogo katika riwaya hii aliathirika kwa sababu ya ubaguzi wa kikabila. kwa sababu hakuwa kabila la mmoja wa viongozi wa polisi, alifanyiwa dhuluma. Mambo kama haya ndiyo hukwamisha nchi na kufanya maisha ya watu kuwa magumu. Bila shaka nchi

haiwezi kuendelea mbele ikiwa watu wenye ujuzi na vipawa vya kazi zao watafungiwa njia ili kuwapisha mabwege wa kabila fulani. Hili ni jambo ambalo linadhihirika wazi wazi katika nchi nyingi katika karne hii ya ishirini na moja.

### **3.2.5 Mataifa yanayoendelea kama kundi la panya wa majaribio**

Mataifa yaliyoendelea wanatumia mataifa yanayoendelea katika tafiti zake. Mataifa yaliyoendelea hulazimisha mataifa yanayoendelea kufuata sera za kiuchumi zilizobuniwa na mashirika pacha ya Benki ya Dunia na Mfuko wa kifedha wa Kimataifa.\*<sup>†</sup> Baadhi ya nchi nyingi Barani Afrika hujipata katika msukumo unaosababishwa na baadhi ya matukio yanayotoka nje. Asilimia kubwa ya matatizo yanayozisakama nchi nyingi, huchangiwa na mashirika hayo.

Sera za mashirika haya zinazojulikana kama mpango wa kubadilisha muundo wa kiuchumi, ndizo zinazochangia mfumo wa kitabaka wa kimataifa. Kwamba kuna mataifa maskini na yale tajiri. Mataifa maskini, Kenya ikiwemo, yalijumlishwa katika jina la kimadharau: Ulimwengu wa Tatu. Ni wazi kwamba nia ya mashirika haya na sera zake ni kupata njia mwafaka kuyawezesha kuyadhibiti kiuchumi mataifa maskini.

### **3.2.6 Watawaliwa kama kundi la vipanya**

Katika sura ya kwanza tuliona kwamba UHU unakiri uwezo kama jambo lenye maana katika uundaji wa usemi. Uchanganuzi hakiki usemi unamulika mahusiano ya uwezo kati ya wahusika tofauti tofauti katika jamii. Uhusiano huu una msingi wake katika utawala. Kikundi

---

\* Haya ni mashirika ambayo yalibuniwa na mataifa yaliyoendelea ili kuyasaidia yale yanayoendelea (World Bank and International Monetary Fund)

kimoja ni cha utawala ilhali kile kingine kinatawaliwa.Wakati mwingi wenye uwezo ndio hutawala.

Riwaya hii inaonyesha wazi kwamba watawaliwa wanatumiwa na watawala kufanya tafiti zao.Waziri Rashid anatumia uwezo wake kutawala watawaliwa kwa njia isiyostahili .Baada ya mwanapathologia wa serikali kutoa taarifa kuhusu maiti ya Rita Kings ,waziri Rashid anatumia uwezo alio nao kutekeleza ufasadi kwa kubadilisha matokeo ili kuonyesha kwamba hakuhusika na mauaji ya Rita.Mwanapathologia anaposhurutishwa kubadilisha taarifa yake hata baada ya kuitangaza anatumika kama kundi la vipanya.

Aidha waziri Rashidi anatumia mamlka yake aliyo nayo kujibizana vikali na wapelelezi wa FBI baada ya habari zilizotolewa na mfanyi kazi wa serikali kuhusu habari aliyoitoa juu ya mazungumzo ya simu baina ya waziri na marehemu Rita. Vilevile Rashidi anahakikisha yule mfanyi kazi wa serikali anauawa ili kuharibu ushahidi wote kwa kutumika kufanywa kundi la vipanya bila yake kushitakiwa hata inapojulikana kwamba ameshiriki kwenye mauaji hayo. Hivi ndivyo watawala hutumia mamlaka yao kutenda watakalo bila kuulizwa lolote.

### **3.2.7 Njia tofauti kutumika kujinufaisha**

Jamii ya *Vipanya Vya Maabara* bila shaka inatumia njia tofauti kujinufaisha huku ikiwafanya wenzao kuwa makundi ya vipanya.Njia hizo ni pamoja na ukahaba ,ukware ,wizi wa kimabavu,usherati na hata mauaji.Sababu kuu ya kuulazimisha jamii ya *Vipanya Vya Maabara* kujiingiza katika njia hasi za kujinufaisha ni ile hali ya viongozi kukosa uadilifu na vitawi vyake kama vile nidhamu,uaminifu,bidii na uzalendo ambao mwandishi anadai kwamba ilikuwa dini isiyokuwa na wafuasi (uk 184). Vilevile sera za kuindeleza nchi zilizotumika na viongozi zilichangia sana katika kuibua nyendo potovu za kujinufaisha.

Sera za serikali za kupunguza gharama kwa kuwasimamisha watu kazi mapema, mpango wa *retrenchment* uliwaathiri wafanyikazi wengi. Wengi wao walitumika kama vipanya vya maabara. Waliofanyiwa utafiti huu hawakufaidika kwani wengine walikua na mikopo ambayo ilikatwa kutoka kwa pesa walizopewa huku wakilazimika kujiingiza katika njia mbovu ili kujikimu kimaisha. Wengi walijiingiza katika ukahaba na wengine walianza wizi wa kimabavu.

Sera za asasi za elimu vilevile zilichangia katika kuukuza ukahaba na usherati. Vijana wengi baada ya kukamilisha masomo ya msingi na ya shule za upili hukosa senti za kujiunga na vyuo vikuu, kwa hivyo hawajaweza kujitegemea hivyo basi kuishia katika biashara za ukahaba, na hata wizi wa kimabavu ili kupata senti za kujikimu kimaisha. Vilevile waliohitimu hawajaweza kupata kazi kwa kukosa ujuzi wa kutosha. Tabaka la akina Rashidi Hamisi ndilo lililoidhibiti maabara ya kitaifa ambamo jamii ya *Vipanya Vya Maabara* ilikuwa vipanya vya kufanyia majaribio. Viongozi hao waliotarajiwa kutoa mfano ndio waliozama kabisa katika maovu.

### **3.3 AINA TOFAUTI TOFAUTI YA VIONGOZI PAMOJA NA MCHANGO WAO**

#### **3.3.1 Waziri Rashid Hamisi**

Kwa kawaida mawaziri wa nchi yoyote ile huwekwa katika daraja ya juu katika uongozi. Mawaziri pamoja na rais hubuni baraza la mawaziri, kitengo ambacho ni muhimu sana katika kuendesha mambo yanayohusu nchi yao. Nyendo na matendo yao hulazimika kuwa ya haki na uwazi katika kutekeleza majukumu yao. Wananchi huwa wana imani kubwa nao kwani

wao ndio huendesha shughuli za kiserikali.Lolote wafanyalo huwafaidi wananchi au kuwaathiri visivyo.

Waziri Rashid Hamisi ambaye ni waziri wa ulinzi ni kiongozi ambaye nyendo na matendo yake yanaleta maendeleo hasi kwa jamii ya *Vipanya Vya Maabara*.Mheshimiwa huyu anawatumia vijana ili kutekeleza majukumu yake, kwa hakika anawatumia kwa utafiti wake huku akiangamiza jamii kwa jumla.Waziri Rashid anamtumia Sweleh kijana mhuni aliyetaalamika katika wizi wa kutumia nguvu kama wakala wake wa kumsambazia madawa ya kulevya ya kokeini.Kazi ya kuuza mihadarati ndiyo inamletea waziri huyu mapesa mengi.Uaziri ni kazi ambayo inamfunika na kumpa uwezo wa kuuza mihadarati.

Swaleh huisambaza kokeini katika vilabu na mahoteli wanakoenda watoto wa matajiri.Vilevile huiuzwa katika mitaa ya Parklands na Pangani ambako kuna wateja wengi wa kihindi. Aidha huuzwa hata vyuoni hasa vile vya kibinafsi.Hii ni hali ambayo inaakisi hali halisi kama ilivyo katika nchi nyingi ulimwenguni.Viongozi ambao ndio hasa huagizia mihadarati hawatiwi mbaroni, badala yake mawakala wao wanaowasambazia pamoja na wale wanaotumia ndio hushtakiwa huku wakiangamizwa kiafya.

Wakati kunatokea juhudi za kuchunguza nyendo na matendo yao,wao hufanya jitihada ili kuwazuia, na hata majasusi wengine huelekea kuangamizwa kabisa.Kwa mfano jasusi Rita King kutoka Marekani aliyetaka kufanya uchunguzi kumhusu waziri wa ulinzi Rashidi Hamisi na kazi alizozifanya aliishia kuuawa na Rashidi mwenyewe.Matendo, maneno na nyendo za kiongozi Rashidi ni mfano unaodhihirisha unafiki wake kuwakandamiza wanyonge.Anatumia uwezo na daraja lake ili kutawala semi pale anapotagusana na wananchi wanaotawaliwa naye.

Van Dijk (1997) katika sura yetu ya kwanza anaeleza kwamba kuna matumizi mabaya ya uwezo, wenye uwezo hupitia usemi kama njia ya kitega uchumi kitiikadi. Hata ingawa UHU inatarajia kwamba wale wanaotawaliwa watie bidii kujinusuru kutoka kwa watawala, jambo hili si rahisi na badala yake watawaliwa huishia kukaidi.

Karibu kila wakati ni kweli kwamba matakwa ya wenye uwezo kijamii hudumu. Kwa mfano waziri Rashidi anamnajisi jasusi, Rita King na baadaye kumuua na kisha kuitupa maiti yake barabarani. Mwanapathologia wa serikali anaifanyia uchunguzi maiti hiyo, uchunguzi unabainisha kwamba marehemu Rita kweli alikufa kwa kunyongwa baada ya kubakwa.

Habari hizi zilikuwa kwenye vichwa vya magazeti yote siku iliyofuata. Lakini la ajabu na kushangaza ni kwamba wakati upelelezi ulipokuwa ukiendelea, yule mwanapathologia wa serikali alijitokeza kwenye vyombo vya habari na kutoa taarifa iliyosema kuwa kamwe hakusema kwamba uchunguzi wa maiti ya Rita ulionyesha kwamba alinyongwa baada ya kubakwa, lakini alilazimishwa kutoa habari nyingine tofauti, kwamba Rita aligongwa na gari ambalo halikusimama baada ya ajali. Huu ni mfano wa jinsi mambo yanavyotendeka nchini huku viongozi wakiachwa huru bila kushtakiwa na hata wanaoshtakiwa hutumia uwezo wao kuachiliwa huru.

Taarifa hiyo ilisisitiza kwamba uchunguzi ulionyesha kuwa marehemu aligongwa na gari ambalo halikusimama baada ya kutenda uhalifu huo. Viongozi wa serikali walihakikisha kwamba rekodi zote za uchunguzi huo zimetoweka. Ufisadi mkubwa ulikuwa umetendeka na ulitendwa na wale wenye mamlaka ya kisiasa waliokuwa wakitatiza jitihada za babake Rita King. Kazi ya seneta Humprey King ikazidi kutatanika na kuwa ngumu. Nyendo kama hizi ndizo hasa husitisha ukweli kupatikana na kurudisha maendeleo nyuma. Seneta Humprey aliamua kwamba angeitumia miaka ya uhai wake yote iliyobaki na utajiri wake wote katika

mradi mmoja tu: kutegua kitendawili cha mauaji ya mwanawe mpenzi. Hata kama ukweli ulipatikana pesa zilizotumiwa kupata ukweli huo zilikuwa nyingi sana hivyo kuhujumu uchumi wa nchi ya seneta Humprey King.

### **3.3.2 Walimu kama viongozi katika asasi za Kielimu**

Majukumu ya walimu hujumlisha zaidi ya kusimama darasani ili kufundisha. Kwa hakika ingawa walimu hutumia muda mwingi wakiwa darasani kufunza, kule kufundisha ni sehemu tu ya kazi zao. Mwalimu aliyeajibika huelewa kwamba kufundisha kunahusu kuvaa kofia nyingi ili kuhakikisha kwamba mwanafunzi anajengeka kikamilifu kiafya, kielimu, kitabia au kisosholojia na kadhalika.

Mwalimu huwa kiongozi ambaye nyendo na tabia zake lazima ziwe za hulka inayoweza kuigwa kama mfano mwema. Wakati mwingine mwalimu huchukua nafasi ya mzazi ili kuwaelekeza wanafunzi katika njia bora na hata pia akawa daktari. Mara nyingi utawasikia wanafunzi wakiwaeleza wenzao kwamba wangependa kuwa kama mwalimu fulani au fulani, ni sharti wawe kielelezo chema cha kuigwa.

Katika shule ya Moi ambapo Wairi na wenzake wanasoma, walimu wanafanya kinyume na yale wanastahili kuyafanya. Badala ya kuwa kielelezo cha kuigwa wao wanawageuza wanafunzi kuwa vipanya vya kufanyia tafiti zao. Mwalimu mkuu wa shule hii amewafanya wanafunzi wa kike wake zake. Kwa mfano uja uzito wa Wairimu ulisababishwa na mwalimu mkuu wa shule yake. Kiongozi wa shule ambaye ana wajibu wa kuwaelekeza wanafunzi na hata walimu kwa jumla hangestahili kutenda uovu huo.



Inaonekana kwamba mapenzi kati yake na mwanafunzi huyu sio jambo la faraghani ni mambo ya wazi kwani hata Wairimu anaposherehekea siku ya kuzaliwa kwake Mwalimu Mkuu haoni haya kumtuma taarishi wake Bwana Nyamboki ili kumwakilisha. Hili ni jambo ambalo liliwashangaza sana vijana wote waliohudhuria sherehe hiyo na hasa pale taarishi wa shule yao anapomkabithi Wairimu bahasha ya zawadi kutoka kwa Mwalimu Mkuu huku akimnong'onezea sikioni.

Mwalimu Mkuu amegeuka zimwi ambalo limeamua kulichafua jina zuri la mwalimu, hali ambayo imechangia sana katika kuwafanya wavulana na wasichana wa shule ya Moi kujiingiza katika mambo ya ukahaba na ukware kwani kule shuleni walimu wa kiume walishindana na wanafunzi wa kiume katika kujishindia wapenzi warembo ambao walikuwa wanafunzi wa kike kina Wairimu, Freda, Jamila na wengine. Na kwa vile walimu hao ndio vielelezo wao sio ajabu kwamba tabia za ukahaba na usherati waliziiga kutoka kwa walimu wao.

Wavulana wengi wa darasa la Bob walipatwa na ashiki ya juu sana. Hawakuweza kushikilia nidhamu iliyohitajika ili kujiepusha nayo. Wengi wao walishamfichulia Bob siri za matembezi yao kwa makahaba. Walizuru madongoporomoka ya Bondeni ambapo makahaba walipatikana, walifanya hivyo baada ya kuwaibia wazazi wao pesa ili kulipia huduma za makahaba.

Nazi mbovu miongoni mwa walimu zilikuwa harabu kwa sifa nzuri ya kazi hii.(uk 88) Maneno na matendo ya walimu yalichangia katika kuwapotosha vijana. Wengi wao walionyesha jinsi walivyoidharau kazi yao wenyewe, wengi walisema waziwazi darasani kuwa waliingia katika ualimu shingo upande. Hii ndiyo sababu ya kuifanya kazi yao ovyoovyo. Kuchelewa kufika darasani, kutojitayarisha kabla ya kufunza, kulewa wakati wa

kazi, kuwa na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi wao. Katika shule ya msingi ya Uhuru kulikuwepo na jozi za wapenzi kama vile Bob na Jamila, Swaleh na Achieng, Okach na Freda, Muli na Wairi. Katika jozi hizo nne, ile ya Muli na Wairi ndiyo iliyotetereka zaidi.

Wairi alishindaniwa na wanaume wengi ambao walikuwa na nguvu mara elfu kumshinda Muli. Ilifika wakati akasalimu amri. Iitokea hivyo wakati Wairi alipotungwa mimba na mwalimu wake mkuu. Ilibidi Muli akajaribu kwingine. Baada ya Wairi kujifungua mtoto wa kiume alilazimika kumtunza na kumtimizia mahitaji yake yote. Hali iliyompelekea kuwa kahaba kazi ambayo iliumbua utu wa mwanamke.

Hawa walimu ambao walihitajika kutoa huduma katika asasi za kielimu walishachoka kulia kwamba ukosefu wa vifaa na sera madhubuti pamoja na malipo duni waliyopata viliwazuia kufanya kazi yao. Wengi walisikika wakisema "...potelea mbali kama nchi haina haja na watoto wake wacha waangamie." ( uk 214 ) Walimu wanawalaumu viongozi kwa kuchagua sera ambazo si bora kwenye asasi za kielimu na badala ya kutia bidii ili kuzirekebisha, wao wanaamua kuitesa jamii yote kwa jumla.

Baada ya wanafunzi wengi kukamilisha masomo ya upili ni wachache mno wanaojiunga na vyuo vikuu ili kuendeleza masomo yao huku asilimia kubwa ikijiingiza katika kazi zisizofaa kwa kukosa ujuzi, kazi ambazo zinazalisha umaskini wa hali ya juu, uhalifu, usherati, ufisadi, ulaghai, wizi wa kimabavu na hata mauaji. Hii ni njia ya viongozi kukiua kizazi cha baadaye huku wakihujumu uchumi wa nchi.

### 3.3.3. Maofisa wa polisi

Kulingana na katiba mpya ya Kenya (2010) sura ya kumi na tatu, ibara ya nne, vifungu vya (a) hadi (e) inaeleza kwa ufasaha kuhusu majukumu ya polisi. Katiba inaeleza kwamba jukumu la huduma ya polisi ni kutoa ulinzi wa maisha na mali, kudumisha amani ya umma na hali nzuri, na kuzuia, kuchunguza na kutatua uhalifu kwa kuwaleta wahalifu katika mfumo wa sheria.

Maafisa wa polisi wana wajibu wa kufanya kazi zao kwa utaalumu na kuonyesha kimaadili tabia katika kila kitu chao. Sheria inasisitiza kwamba polisi wasiwe na ubaguzi dhidi ya mtu yeyote kwa misingi ya rangi, taifa au kikabila asili, lugha, dini, jinsia, umri au kimaumbile. Kwa hivyo wanastahili kuwajibika.

Inspekta wa polisi Kamash wa kituo cha Mjinikati alikiuka sheria kwa kufanya kinyume na alivyostahili kufanya. Maneno na matendo yake yanadhihirisha unafiki wake. Badala ya kupunguza au kuzuia uhalifu anauzidisha huku akiwaingiza vijana katika jinamizi la kifo kwa tamaa yake.

Polisi kamash badala ya kutumia bastola kuilinda jamii anawakodisha vijana ili kuitumia katika kutekeleza uhalifu na hasa uporaji wa kimabavu. Uhalifu unaonyeshwa wazi wakati Bob anamkuta rafikiye Swaleh kwenye kituo cha magari ya kuelekea Meru, Embu, Chuka na Maua akimsubiri kamash. Alipoulizwa alichokuwa akikifanya alisema, (uk182) “Ninamsubiri ofisa Kamash ili tuelekee kwenye mpango wetu.” Bob hakushindwa kuelewa ni mpango upi. Alitumia mkakati wa kudhihirisha nguvu za usemi kupata uzito wake ambao ulifichwa kidogo.

Swaleh anaongezea kwa kusema kwamba “Leo lazima nipate kwani kuna Mhindi wa Parklands ambaye alitoa pesa benki na tutamtembelea leo na ikiwa hataleta ujinga tutamuachia roho yake.” Maana ambayo Swaleh aliificha ilikuwa kutekeleza wizi wa kimabavu kwa kutumia bastola. Vilevile ikiwa mhindi angekataa kuwapa pesa wangemtoa uhai. Badala ya ofisa Kamash kuwafunza amani aliwaingiza katika uhalifu na kusababisha Swaleh kuuawa. Aliwatumia kama vipanya katika utafiti wake.

Ubaguzi na ukabila ni mambo ambayo yanamulikwa sana katika idara ya polisi lakini katika riwaya hii viongozi wa polisi wameyapuuza na kuonyesha mapendeleo. Konstebo Kerogo ni mmoja kati ya maafisa wa ngazi za chini ambao haki zake zimekiukwa na wakubwa wake. Idara ya polisi hapa inaonyesha nyendo zinazosababisha dhuluma kwa maafisa wa daraja la chini. Sababu kuu ya kubaguliwa ni hali ya uwazi waliyo nayo. Hawaogopi kusema ukweli, jambo ambalo wakubwa wao hawalipendelei.

Konstebo Kerogo anajulikana kwa uhodari wake na vilevile kwa uwazi wake. Ni ofisa ambaye haogopi lolote, yeye husema ukweli na kutenda yanayostahili. Wakubwa wake ambao wanajivunia ufnisadi hawampendelei Kerogo. Anakandamizwa kwa kutopandishwa cheo kwa miaka mingi aliyohudumu kama polisi. Wale wote wanaokuja nyuma yake na aliowafundisha kazi ya polisi, wanamuacha katika ngazi ile ile ya konstebo.

Hali hii bila shaka ndiyo ilimfanya Kerogo kukata tamaa ya maisha. Inamlazimu kuingilia ulevi wa kupindukia, anaitelekeza familia yake ambayo hapo mwanzoni aliishughulikia kwa hali na mali. Kerogo anasikika akisema kwamba,

Kaeni na-navyo. Hik! vyeo vyeenu Hik! Sheenzi. Majambazi.

Wakabila. Miimi ni Kerogo wa Imathio. Hik! Sitiishwi na mtu.

Nita... hik! Seema ukweeli waazi! Cheo? Miimi hunywa na kula cheo? Siraambi matak... hik! ... ya wakuubwa. Kaeeni na vyeeo vyenu. Hik! Kazi ya polisi nayo ni kazi? Siitaki. Hik! Sijaali tena. Miaka yoote hii hakuuna chochoote... Dhuluma tupu. Hik!.. Anajali nani nchi hii? Hik! Ukaabila, mapendeleo na uufisadi kiila mahaali. Hik! Taakataaka! ( uk 29 – 30)

Kerogo ametamauka kwa sababu ya hali hii iliyosababishwa na viongozi wake. Familia yote ya Kerogo imeangamizwa kwa sababu ya dhuluma aliyofanyiwa baba yao. Dhuluma za aina hii ni mfano wa mambo mengi yaliyoikwamisha nchi na kuyafanya maisha ya watu yazidi kuwa magumu. Watu wengi wenye uwezo na vipawa vya kazi zao wanafungiwa njia ili kuwapisha mabwege wa kabila fulani, na kurudisha maendeleo nyuma. Hali kama hii huzidisha mivutano ya kikabila na hivyo kuhakikisha kwamba umoja wa kitaifa haumei mizizi.

Mkakati mkuu ambao unatumiwa na viongozi hawa ni kupuuza hisia na maoni ya wananchi kuhusu jambo lolote njia ambayo Van Dijk (2008:85) anaeleza ndio njia inayotumiwa na viongozi ili kudumisha uwezo wa kijamii na kuweza kutolewa upya bila kupingwa.

#### **3.3.4. Wazazi kama viongozi nyumbani**

Familia ndiyo kitengo cha kimsingi katika maisha ya mwanadamu katika asasi za jamii, wao ndio huwa nguzo ambazo huhimili wanajamii wote. Wao vilevile hutumika kama vielelezo vyema vya kuigwa na jamii nzima na endapo watalegea katika majukumu yao ni sharti

familia itaangamia. Mara nyingi wazazi wengi hujishughulisha kutafuta pesa huku wakisahau majukumu yao ya malezi na maelekezi ya wana wao

Katika riwaya hii Wairimu ni mmoja wa wanafunzi ambaye tangu utotoni alijilea mwenyewe. Ni wazi kwamba wazazi wake waliwajibika kikamilifu kwa upande wa karo, chakula, mavazi na pesa za matumizi lakini hawakuwa na wakati wa kutoa maelekezo na ushauri. Wairi alikuwa na uhuru mkubwa wa kufanya alivyopenda.

Wakati wa kusherehekea siku ya kuzaliwa kwake wazazi wake hawajishughulishi na mipango yake. Mambo yote anajipangia, anawaalika wageni jinsi apendavyo hata na mpenzi wake na jozi za wapenzi wa shule yake. Sherehe zinaendelea hadi usiku bila ya wazazi wake kuwepo. Utepetevu wa wazazi wake unachangia katika utovu wa nidhamu unaomkumba.

Ingawa wazazi wa Jamila wanaajibika katika shughuli zao za ualimu na vilevile katika dini ya Uisilamu ambayo haiwaruhusu kamwe kuingiliana na watu wasiokuwa Waisilamu na hasa Bob aliyekuwa Mkristo, lakini wamechangia pakubwa katika kumpotosha mwanao Jamila. Kuna wakati walipofunga safari kwenda Mombasa kuhudhuria harusi ya shangazi wake Jamila. Wakati huo walimuacha Jamila peke yake ili aitunze nyumba yao kwa muda wa siku mbili. Iliwalazimu kumuomba ruhusa ili asihudhuria masomo bila kujua kwamba hapo ndipo walimuacha aliwe na simba.

Wakati huo alipata nafasi ya kumualika mpenzi wake Bob ili ampe zawadi aliyomuahidi atampa mara tu atakapofika umri wa miaka kumi na mitano. Jamila alitaka kumuonyesha Bob kwamba sasa alishatoka utotoni na kuingia katika ujana yaani utu uzima.

Bob alitatizika sana kwani hakuelewa ni zawadi gani ingemfanya kuwa mtu mzima. ( uk 59)  
“Mtu mzima wapi? Mi nayajua maisha yako. Bado hujafika utu uzima mpaka upate zawadi yangu”. Jamila alisema. Zawadi ya Bob ilikuwa kwamba Jamila avunje ubikira wake kwake Bob. Hili ni jambo ambalo lingezuiliwa ikiwa wazazi wake Jamila wangeajibika.

Muli vilevile aliachwa kuelea ulimwenguni tangu akiwa mdogo. Walezi wake walikuwa kokeini na makahaba. Tabia ambayo aliiga kutoka kwa mamake kwani alizoea kubadilisha wanaume kila siku hasa maofisa wa polisi. Kisha Muli alipewa elimu ya shuleni ambayo ilimwambia lazima awe fundi na mwanasayansi, ajue kila kitu na apite yote kwa alama za juu. Haikushangaza kwamba Muli alishindwa na yote hayo, akaishia kufa mapema.

Hawa walikuwa tu ni baadhi ya vijana wengi walioishia kuangamia kwa kukosa malezi mema ya wazazi wao ambao walistahili kuwaongoa badala ya kuwatelekeza. Ilikuwa kweli kwamba (uk 165) “Watoto wa Nyayo wameanza kupunguka sasa ndipo kizazi chetu kinaanza kuvuna matunda machungu ya malezi tuliyopata na majaribio ya kiendawazimu ambayo tumefanyiwa maishani,…” Okach alisema. Hali hii inadhihirishwa na jinsi vijana wengi wanaonekana kuwa katika hali ya kutamauka kwa kukosa ajira .

### **3.4.Hitimisho**

Katika sura hii ya tatu, tumechanganua maudhui kuhusu makundi tofauti tofauti ya vipanya vya maabara. Kilichotupa msukumo wa kuteua maudhui ni kule kutokana na umuhimu wake katika kuainisha aina ya viongozi na mambo wanayoyatekeleza ambayo ni muhimu kwa kazi hii.

Kutokana na maudhui kuhusu makundi ya vipanya tumeweza kutambua nyendo na tabia za viongozi ambazo zimedhihirisha unafiki wao. Tumeona jinsi makundi ya vipanya yametumiwa katika tafiti tofauti tofauti ambazo badala ya kuinufaisha jamii imeiangamiza. Nia ya tafiti hizi ni viongozi kutaka kujinufaisha na kutosheleza haja zao bila kufikiria athari zake. Katika riwaya hii, tumeona kwamba viongozi wana uwezo mkubwa wa kudhibiti maisha ya wanyonge na hufanya hivyo kwa kutumia mikakati tofauti tofauti ikiwemo udhibiti wa usemi na vilevile madaraka waliyo nayo.

Tumeona pia kwamba ubishi umetumiwa na baadhi ya viongozi kupitia mikakati ya ubaguzi, uonevu na hata ukandamizwaji kuendelezwa kwa kuwanyima watu wa daraja za chini haki zao. Hata hivyo watawaliwa hao wametia bidii kujinusuru ingawa wengi wao hawakufaulu lakini Bob na Seneta Humphrey King walifaulu kwa kukaidi jambo ambalo uchanganuzi hakiki usemi inatarajia uwepo hata kama hautafaulu. Imedhihirika kwamba matendo ya viongozi hayaonyeshi maadili ya jamii.



## SURA YA NNE

### UCHAMBUZI WA MAUDHUI NA WAHUSIKA KATIKA *MAJIRA YA TUFANI*

#### 4.0 UTANGULIZI

Sura hii ya nne tumeichunguza na kuichanganua riwaya ya *Majira Ya Tufani* ambayo imeandikwa na mwandishi yuyo huyo aliyeandika *Vipanya Vya Maabara*. Sababu kuu ya kutumia riwaya hizi mbili ni ili tuweze kupata ithibati ya kutosha kuhusu tathmini yetu.

Tumechanganua maudhui kuhusu jamii ya Wananakada jambo ambalo limetufunulia yale yanayoihusu riwaya hii na kutuelekeza katika kutambua jinsi viongozi wa Wananakada walivyosababisha mabadiliko ya *Majira Ya Tufani* na sababu mahususi ambazo kwa kiwango kikubwa zimechangiwa na hali ya mabaki ya kikoloni iliyoathiri Wananakada.

#### 4.1 Muhtasari wa *Majira Ya Tufani*

*Majira Ya Tufani* ni riwaya ya kitashititi inayotumia kinaya, vichekesho na mbinu nyingine anuwai kumulika jamii ya kisasa na changamoto zake. Riwaya hii inayahusu makundi mbalimbali ya kijamii yenye imani na itikadi zinazotofuatiana vikali. Baadhi ya makundi hayo ni kama vile wakwasi na wahasimu, tabaka la juu na lile la chini, watawala na watawaliwa, wafalme na watumwa, tajiri na maskini baina ya makundi mengine.

Mivutano hii ambayo imeathiri jamii ya Wananakada na hata Wanauketa nusura iiangushe dola, inatiliwa nguvu na uhalifu na unyang'anyi wa mali ya umma unaofanywa na meya wa Nakada Macho wa Tatu pamoja na balozi wa Ukwadini Balozi Prince aliyeteuliwa na nchi

yake kuja mataifa maskini kama Uketa ( Uganda, Kenya na Tanzania) kudumisha utabaka wa kimataifa.

Uongozi hafifu na uhafidhina vilevile umechangia pakubwa katika mvutano huo hali ambayo bila shaka imechangiwa sana na mabaki ya Kikoloni. Yote haya yamewasilishwa kupitia hadithi ya kulisimua inayomvuta msomaji kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi yenyewe.

## **4.2 Upambanuzi wa Maudhui Kuhusu Wananakada**

Uchambuzi wa maudhui kuhusu Wananakada ulituwezesha kutambua sababu zilizoipelekea jamii hii kujiingiza katika mivutano. Jamii hii ambayo ilibandikwa jina la wahasimu, ilileta mivutano kwa sababu ya kutetea haki zao zilizokiukwa na wale Wakwasi na viongozi wao.

### **4.2.1 Ukoloni na Ukoloni Mamboleo.**

Kwa mujibu wa kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004) ukoloni ni mtindo wa nchi moja kuitawala nchi nyingine, nao ukoloni mamboleo ni mfumo wa utawala wa nchi za Kibepari kuwa na ushawishi mkubwa wa kiuchumi katika nchi zinazoendelea kwa maslahi yao. Yaani hali ya kukosa usawa wa hali ya juu baina ya watawala na watawaliwa. Watawala wanakuwa wagandamizaji, na watawaliwa ni wanyanyaswaji. Tatizo ambalo kuibadilisha mifumo hii haiwezekani na hata ikiwezekana huleta matatizo magumu zaidi.

Katika riwaya hii ukoloni mambolea ndiyo chanzo cha Uhasimu unaodhihirika katika kazi hii. Nchi za Ukwasi zilitumia maswala ya utandawazi kama kisingizio cha kuzinyanyasa nchi maskini kiuchumi. Nchi maskini ambazo zinaendelea zilichukulia kwamba utandawazi

uliashiria mshikamano wa kiuchumi wa kimataifa ilhali ilikuwa njia tu ya kuvutwa kwa chumi za mataifa mengine kuingia katika himaya ya Ukwadini nchi ambazo zilikuwa zimeendelea, njia zilizoonyesha wazi wazi unafiki.

Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao katika nchi maskini ndio wanaotumiwa kuudumisha utabaka wa kimataifa. Wao huwatumia viongozi katika kutekeleza ulaghai.

Riwaya ya *Majira Ya Tufani* inatoa mfano wa kiongozi aliyeshinikizwa kuudumisha ukuloni. Mheshimiwa Meya wa Nakada, Macho Wa Tatu ni kiongozi ambaye matendo yake yanaonyesha kuunga mkono ukuloni mambolea. Ni kiongozi ambaye alizaliwa na familia ya kifalme na kisha kwenda katika nchi za magharibi kwa masomo yake. Alipojiunga na chuo kikuu kule Ukwadini alipata mchumba wa rangi nyeupe ambaye alifunga ndoa naye. Mchumba huyu alikubali kwa sababu ya utabaka wao. Wote wawili walihusika na tabaka la juu. Hali hii ilimbadilisha Macho wa Tatu kumfanya awe na fikra na nyendo za Ukwadini. Viongozi ambao walikuwa na dharau kwa Wanauketa.

Wakati wa sherehe ya ufunguzi wa jumba la *Macho Plaza*, Macho Wa Tatu aliwaalika viongozi mbalimbali. Kulikuwa na mawaziri, balozi na vilevile Wanauketa. Jambo lililoshangaza sana ni kwamba wageni walipowasili walisalimiana kwa uzuri na furaha. Lakini Balozi wa Ukwadini alipowasili alimsalimia tu Meya Macho wa Tatu na kisha kuwapuuza viongozi wengine. Balozi Dan Prince alisema,

Waziri kitu gani mbele ya balozi wa taifa la Ukwadini?

Meza sawa. Ana uhusiano wa kipekee na taifa letu. (uk 7)

Maneno haya kutoka kwa kiongozi yule yalionyesha kwamba, uwezo alio kuwa nao ulikuwa mkubwa sana hivi kwamba viongozi wengine walionekana kama watu wasiofaa. Mkakati alioutumia ni ule wa kurejelea. Vilevile anaposimama kutoa hotuba yake anawarejelea matajiri kama Wakwasi wenzake huku akionyesha wale Wanauhasimu (maskini) dharau.

kama alivyosema mwenyewe Mheshimiwa Meya, amefanya jitihada kubwa, ametumia fedha nyingi kufikia hatua ya kuukamilisha mradi huu. Na kwa kuukamilisha, amethibitisha kwamba yeye ni mfuasi wa dini yetu ya Ukwasi. Naomba niwakumbushe mojawapo ya nguzo zake. Nayo ni kwamba binadamu ana jukumu la kuchapa kazi ili kutafuta utajiri. Utajiri ni kipengele cha uungu, alisema kwa msisitizo. (uk 12-13)

Balozi yule aliwarejelea wale wa tabaka la chini kama mahasimu ambao dini yao ni ugaidi na ushenzi. Wanauketa hawakufurahishwa na maneno ya Balozi Dan na kwa kukaidi walizua vurumai na kumshambulia balozi kwa makombora na matusi. Alikatizwa ghafla na sauti kuu zilizotoka katikati ya umati.

Astaghafiru, kakufuru!

Cheichei, matukano!

Hasha lillah! Hayavumiliki tena!

We ndiye mshenzi hasa!

Mbaguzi wa kimbari!

Mnafiki mkuu!

Kufia mbali! (uk 13)

Zilikuwa sauti kali zilizojaa ghadhabu. Hivyo ndivyo Balozi Dan Prince alivyoona cha mtema kuni kutokana na maneno ya hotuba yake ambayo ilikatizwa kabla hajaimaliza. Hali

kama hii ya watawaliwa kukaidi hata kama hawatafaulu ndiyo inahimizwa na nadharia ya uchanganuzi hakiki usemi. Kwamba watawaliwa kila mara watie bidii kujinusuru kutoka kwa utawala huu, Van Dijk (1997).

#### **4.2.2 Ufisadi.**

Ufisadi ni aina yoyote ya maovu au uharibifu. Wakati mamlaka au madaraka yanatumiwa ili kumnufaisha mtu binafsi au kundi la watu, vilevile huo ni ufisadi. Madhara ya ufisadi huwa makubwa sana kwani umma na serikali hupoteza pesa nyingi kupitia njia zisizofaa. Mara nyingi ufisadi huwaumiza watu wa tabaka la chini na wale wanyonge.

Riwaya hii kwa hakika imeliangazia jambo la ufisadi kwa kina. Kwa hakika ufisadi uliotekelezwa na mheshimiwa Meya wa Nakada Macho Wa Tatu ndio hasa unaanzisha uhasama katika jamii ya Wananakada. Wanaukwasi walimsaidia Meya kuifisadi nchi yake na hasa Balozi Dan Prince. Kwanza kabisa macho alinyakua ardhi ya umma iliyotengwa kwa minajili ya kukijenga chuo cha Uhasimu ambacho kingelea mafunzo ya dini na pia kazi mbalimbali kwa Wananakada.

Kiongozi huyu anatumia njia ya kuwapumbaza Wananakada kwa kusema kwamba jengo la *Macho Plaza* litakuwa fahari kwa Wananakada wote na vilevile kuipa hadhi jiji la Nakada. Meya Macho antumia ujanja kwa kuwahakikishia Wananakada kwamba *Macho Plaza* ni jengo la umma na litawafaidi Wananakada wote, anaonyesha unafiki wa hali ya juu. Mradi wa jengo hilo ulichukua miaka mitatu kukamilika. Macho Wa Tatu alisikika akisema kwamba mradi huu ndio uliokuwa mama wa miradi yake ya kibiashara. Kusanifiwa na kujengwa kwake kulifuata mkondo uliozoeleka nchini Uketa. Nao ni kwamba kitu chochote kizuri lazima kiagizwe kutoka nje, hasa Ukwasini.

Wasanifu mijengo waliolisanifu jengo hilo walitoka Ukwadini. Mafundi waliolijenga walitoka Ukwadini. Saruji, vyuma, vioo na vigae vilivyolijenga vilitoka huko Ukwadini. Sio kwamba vitu hivi havingepatikana Uketa, vilikuwepo kwa wingi. Lakini ilibidi mwenye jengo afuate sheria kuu isiyoandikwa ya utandawazi. Iisema kwamba ukiwa nchi maskini wewe ni soko tu la kupokea vitu kutoka nchi tajiri. Hali hii bila shaka ndiyo imekithiri sana humu nchini Kenya na hata katika mataifa mengi ya Afrika.

Kiongozi Macho anaakisi sifa za uongozi mbaya tulizozijadili katika sura ya pili. Baada ya kutumia mali ya serikali kulijenga jengo hilo la umaarufu anatumia uwezo wake na kubadilisha hati za umiliki wa kile kiwanja cha ekari mbili ambapo *Macho Plaza* inasimama, kisha anatia mfukoni mamilioni ya pesa zinazotokana na kodi inayotozwa waliokodisha vyumba pale. Meya Macho anasababisha umasikini na ufukara kwa Wananakada na nchi ya Uketa kwa kuvuna bila kupanda. Nchi ya Uketa bila shaka inapoteza pesa nyingi huku ikizifaidi nchi za Ukwadini kwa kuagiza mali ghafi kutoka Ukwadini badala ya kutumia inayopatikana nchini ili kupunguza gharama.

Ni wazi kwamba kuna sababu nyingi za nchi za Kiafrika kuchekwa na mataifa yaliyostawi. Zinachekwa kwa sababu ya kuwa zina maliasili nyingi na wakati huo huo kukwama katika umasikini wa kujitakia unaoletwa na viongozi wafisadi. Viongozi ambao pengine hata hawastahili kuwepo katika nyadhifa walizopewa mradi awe ametoka kabila moja na rais wa nchi yoyote ile.

Jambo la kuwateuwa viongozi kwa misingi ya ukabila ni jambo ambalo hata leo hii linarudisha mataifa mengi nyuma. Jambo hili linawafanya wale walio na ujuzi na uelewa wa kazi zile kutupwa nje. Kwa mfano katika riwaya hii waziri wa fedha ni kiongozi ambaye

hakutaalamika katika mambo ya fedha na uchumi, alikuwa mchunguzi wa maiti jambo ambalo lilifanya Uketa kuchekwa na mataifa yaliyostawi kwa unyamavu wake wa kutoitetea nchi yake, sababu zikiwa eti alitangamana sana na maiti hadi akaambukizwa unyamavu. Ufisadi wa aina hii ungepunguzwa kwa kuwateuwa viongozi kwa misingi ya kiwango cha elimu na ujuzi unaostahili katika nyadhifa husika ili kuendeleza nchi mbele.

Njia ya kuwachagua viongozi ilikumbwa na ufiisadi wa hali ya juu sana hadi kuwaathiri Wanauketa ili kuuona kama kwamba ilikuwa jambo la haki kuwachagua viongozi kwa misingi potovu. Kweli kiongozi Macho alikuwa na pesa za kutosha za kununua uongozi. Akisifia umuhimu wa pesa katika uchaguzi wakati wa kampeni alizoea kujigamba kwa kusema kuwa,

kitu ambacho pesa hazikuweza kununua kilikuwa  
uhai. Vitu vingine kama uongozi vilipatikana kwa  
urahisi bora uwe tu na pesa za kutosha. (uk 108)

Usemi kama huu unadhihirisha nguvu za usemi na una uzito ambao umeficha maana. Kwamba fukara hana uwezo wa kuwa kiongozi, utajiri kila mara humithilishwa na uungu lakini pengine mkabala wa Macho wa Tatu ulichangiwa na dini yake. Dini ya Macho ilibeba mbegu za utamaduni wa uzunguni ilikotoka. Hali ambayo Macho aliiga akiwa Ukwadini. Viongozi wengi katika karne hii wamepiga hatua zaidi katika uigaji huu, utawasikia wengi wao wakijigamba kwamba Mungu amewabariki wakapata mali.

Ukoloni mamboleo kwa hakika ndiyo sababu ya kuzuku kwa uhasimu. Balozi Dan ndiye aliyepanga utunzi wa kikosi cha operesheni fukuachapa. Aliwatumia Meya Macho na kamishna wa polisi ili kuwashinikiza wakitunge kikosi hicho, akiwa na nia ya kuwaangamiza

Wanauketa badala ya wao kupata haki zao. Yeye ndiye aliyekuwa mshauri wa serikali, alitaka Macho aweze kukabiliana na magaidi (kama alivyowaashiria) kwa kutumia vyombo vya usalama.

Ilijulikana wazi kwamba mbegu za ugaidi zilipandwa na viongozi wa kisiasa na mawakala wao wa Ukwadini. Kisha viongozi wetu wakazipalilia kwa dhuluma, unyonyaji, uvunjaji haki za wanyonge na hii ndiyo sababu za kushindwa kuimaliza ugaidi katika nchi nyingi zinazoendelea.

#### **4.2.3 Udhalimu kwa Wananakada.**

Kuna mambo ya uonevu, hiana na hata ukatili yanayofanyiwa Wananakada na wale watawala. Mambo yanayokiuka haki za Wananakada yanayoonekana kupita mipaka baada ya wao kutoa vurugu ili ardhi iliyotengewa umma iliyonyakuliwa irudishwe. Udhalimu unaletwa na wale wanaopenda kuchovyachovya ambao wako uongozini. Wanataka waile asali yote wao peke yao ama kweli mchovya asali hachovyi mara moja au kama wasemavyo wengine, "mchovya asali huchonga mzinga"

Baada ya tetezi za Wahasimu kama walivyobandikwa na wale Wakwasi kudai ardhi yao, mambo yalizidi kuharibika. Viongozi wa serikali na idara ya polisi ilitangaza vita dhidi ya magaidi na kinara wao waliokaidi kwa kumteka nyara Lulu mtoto wa pekee wa Meya wa Nakada. Walifanya hivyo ili kumlazimisha Meya wa Nakada kuirudisha ardhi yao. Kasila mmoja wa wahasimu alifafanua pindi Lulu alipotaka kujua sababu za kutekwa nyara kwake kwamba,



Nitakueleza kila kitu ili kukuondolea wasiwasi.  
Babako alinyakua ardhi ya hekalu laUhasimu jijini.  
Alitumia wadhifa wake kama Meya wa Nakada  
kutekeleza wizi huu.Tunataka arudishe ardhi hii  
kwa sababu ni mali ya Uhasimu. Akirudisha kipande  
cha ardhi kinachohusika, sakata hii itaisha hapo.

(uk 78)

Ingawa Lulu vilevile alituhumiwa, jambo la kumteka nyara lilisababisha maafa, ubakaji na vita dhidi ya Wananakada maskini.Kamishna wa polisi aliunda kikosi maalum kwa jina Operesheni Fukuachapa. Oparesheni ya kumsaka Lulu ilipoanza mji mkuu ulikuwa kama uwanja wa vita. Vilio vya wanyonge vilihanikiza, damu ilitiririka katika mtaa wa Mwembeni, watu watano walipigwa risasi na kuuawa na polisi.Polisi wawili vilevile walikuwa wameuwa.Waliuawa na wananchi waliokuwa na ghadhabu baada ya wao kumuibia mjane mmoja pesa zake na kisha kumbaka.

Kwa jumla polisi badala ya kutoa ulinzi kwa wananchi na kuilinda mali yao, waliwageuka raia na kuwafanyia dhuluma ambazo ziliwaacha wengi wakijiuliza ikiwa polisi hawakuwa tofauti na Waketa wengine lakini matendo yao yalikusiana kwa njia nyingine na matukio ambayo yalitendeka awali kama wanavyoeleza Wodak na Hudwig (1999: 12 -13), kwamba nguzo ya mahusiano inahusu uwezo na itikadi na kwamba matukio yaliyotendeka awali yanaweza kuathiri yale ya sasa.

Sababu za polisi kuwa na unyama kiwango cha kutokwa na utu ililetwa na hali yao ya kikazi: Kuajiriwa, kupandishwa cheo na kuwezesha kufanya kazi kulitawaliwa na mapendeleo, ukabila na utoaji hongo. Waliishi kinyama katika vyumba vibovu vilivyokuwa na

msongamano kama ule wa nyuki katika mzinga. Mshahara waliolipwa ulikuwa ujira wa kitumwa. Hivyo basi hali ya kuwa na utu haungetarajiwa kutoka kwao na ndio maana Fairclough na Wodak (1997) wameweka wazi kwamba usemi unajumuisha taarifa, utambulisho wa jamii na mahusiano ya kijamii kati ya vikundi vya watu. Yaani UHU humiliki mahusiano ya uwezo kati ya wahusika tofauti tofauti katika jamii.

Dhuluma nyingine iliyofanyiwa wanyonge ambayo viongozi walihusika nayo ni kule kupandishwa bei kwa nauli ya matatu za kuelekea Mwembeni walikokaa kina yahe. Kijakazi wa Macho wa Tatu alijitwika mzigo mzito wa kwenda Mwembeni ili kumnusuru Lulu. Alipoabiri matatu za kwenda kule, nauli ilikuwa imepandishwa maradufu, jambo ambalo liliwakera abiria wote lakini hawakuwa na la kufanya ila kufyata mikia na kusalimu amri. Walitoa pesa na kulipa nauli huku wakiguna na kulalamika. "Laiti wanyonge wangukuwa na mwamko wa kupigania haki zao kwa umoja. Pengine viongozi wao waliolala kazini wangeamka na kuwajibika. Mambo yangebadilika." (uk 111)

Wanyonge wanaonyesha hali ya kutamauka na kukosa imani kabisa kwa viongozi wao ambao ndio wagavi wa petroli na ndio hasa waliohusika katika kupandisha nauli kwa sababu ya kupandisha bei ya petroli.

Jambo linalowahuzunisha sana wakazi wa Mwembeni ni kule kufanyiwa ulaghai na viongozi wao. Baada ya kijakazi cha Macho kumuokoa Lulu, Macho wa Tatu alitoa ahadi kwamba angetoa fidia ya kuilipia ile ardhi aliyonyakua hata ingawa Wananakada walitaka aibomoe *Macho Plaza* na kuwarudishia ardhi yao. Jambo alilolifanya huyu Meya wa Nakada ni kuwapumbaza kwa kuwalagai. Mke wake alipouliza mchezo atakaouchezea jamii ya Nakada ulikua upi Macho alifafanua.

Tutawacheza hawa mbwamwitu.Macho alijibu.  
Kiwanja cha kwanza na cha tatu ni mali ya  
Halmashauri ya jiji.Cha pili ni cha polisi kamishna  
aliniambia kwamba ujenzi utanza miezi mitatu ijayo.  
Basi mchezo...huu. Fidia tutakayotoa kwa wale  
magaidi ni ya kile kiwanja cha polisi. Mambo  
ya polisi yanahusu serikali. Tutawapa makaratasi  
yasemayo kuwa kiwanja ni chao wakijaribu  
kujenga vitakataka vyao hapo watapambana na  
polisi.(uk 133)

Mke wake Macho alimpongeza huku akidai kwamba hilo lilikuwa wazo la Kifalme. Hivi ndivyo wananchi hudhulumiwa na serikali. Wao husema kwamba ni haramu ardhi yoyote ile kuwa na hati mbili zinazofanana lakini kiongozi aliweza kupata hati nyingine aliyotumia kuwalaghai wananchi. Huu ulionyesha unafiki wa hali ya juu. Macho alitekeleza mpango wake kwa kasi na pia kwa uangalifu mkubwa. Liliishia kuwa jaribio kuu la uwezo wake kama Meya wa mji mkuu, tajiri mkubwa, mfalme wa kabila lake na Mketa Mashuhuri aliyetangamana na wakuu wa nchi. Ilibidi aibuke akiwa mshindi lakini kwa kutumia unafiki wa hali ya juu kuwalaghai wananchi wa uketa jambo lililowarudisha Wanauketa nyuma kimaendeleo.

#### **4.2.4 Ubarakala au Ukabaila**

Ni wazi kwamba makabaila au mabarakala huamini kwamba wao tu ndio hustahili kufaidi kwa njia yoyote ile na kitu chochote kuliko wengine. Wao hujihisi kama kwamba ni viumbe

maalumu kuliko watu wa kawaida. Mara nyingi makabaila huona kwamba hakuna wengine wanaostahili kuwa navyo isipokuwa wale wa nasaba yao, pengine wao huamini wamezaliwa tofauti na watu wengine.

Makabaila hutumia njia yoyote ile ili kuwabagua viumbe duni. Huhakikisha kwamba uongozi ni wao, huwanyima wenzao haki zao, hunyanyasa, kwa hakika hujitakia mambo yote mazuri huku wenzao wakifadhaika.

Katika riwaya hii kuna makundi ya watu ambao wangestahili kuwa viongozi wakuheshimiwa lakini nyendo na tabia zao zinadhihirisha ukabaila. Kwanza kabisa kuna viongozi wa shirika la jeshi ambalo kwa unafiki wao waliwahadaa baadhi ya watu kutoka familia maskini. Shirika hili linatangaza nafasi za kazi ya uhazili. Cha kutia hofu zaidi ni kwamba wale waliotaka kuomba kazi hiyo walilazimika kulipa pesa za mahojiano.

Baadhi ya waliohojiwa, alikuwa mamake Penzi, Mwanauketa aliyekuwa hana mbele wala nyuma, maskini hohe hahe. Baada ya mahojiano alipokuwa anatoka, ofisa mmoja alimfuata nje na kumweleza kwamba angetaka waonane baadaye. Mamake penzi alifurahi huku akiwa na matumaini kwamba angemweleza kuhusu mahojiano yale. Walipokutana jioni baada ya mamake penzi kuuliza ikiwa alifaulu kuipata kazi, ofisa baada ya kuangua kicheko alijibu kwamba,

Mahojiano yalikuwa kitendo cha  
kutimiza masharti ya kazini. Wote  
waliohojiwa wangeambulia  
patupu. Wakubwa wake walikuwa  
washawapa jamaa na marafiki zao  
kazi hizo kwa mapendeleo. (uk 185)

Viongozi hao bila shaka wameonyesha sifa za kutowadhamini wenzao, hili ni tatizo ambalo linastahili kurekebisha ili kuilinda jamii ya leo kutokana na walaghai na wanafiki.

Nakada kama ilivyotambulikana katika riwaya hii ndiyo yaliyokuwa makao ya serikali ya Uketa. Ilikuwa na sifa zote za mji mkuu wa Kiafrika lakini ilikuwa na sehemu mbili ambazo zilikuwa vinyume. Kulikuwa na sehemu moja iliyokuwa na miundo msingi bora, huduma zote muhimu na mazingira nadhifu. Karibu na kitovu hiki kulikuwa na mitaa michache ya kifahari. Viongozi kama vile Meya Macho, Mabalazi wa nchi za nje kama vile Dan Prince na viongozi wote wa serikali waliishi huku.

Ingawa sehemu hii iliishi asilimia ndogo tu ya Wanauketa, pesa zilizotumika kuiboresha sehemu hii zilikuwa nyingi mno. Sehemu ile ya pili iliyochukua asilimia kubwa ya Wanauketa na ambayo ilikuwa mbali na kitovu cha jiji lilitapakaa mabanda, majengo uchwara vilima vya takataka na mito ya maji taka. Miundo misingi ilikuwa haba, na huduma za kimsingi zilikuwa adimu. Asilimia sabini ya Wanauketa walioishi katika eneo hili ndio hasa waliofanya kazi zilizozalisha pesa ambazo zilitumika katika Kitovu cha jiji la Nakada walimoishi manyapara, na viongozi na vilevile Wazungu walioendesha mfumo wa utawala wakati wa ukoloni.

Wengi wao waliwafanyia viongozi wale kazi usiku na mchana ili waweze kujikimu. Ilikuwa hali iliyofadhaisha lakini ilichukuliwa kuwa ya kawaida kwa sababu ubepari ulielekea kukubalika. Hali kama hii ndiyo inayopatikana katika nchi za Afrika ya Mashariki kama tulivyojadili katika sura ya pili. Katika nchi ya Tanzania tulishuhudia mfumo ya Ujamaa ambao ulifeli, Uganda nayo mfumo uliojulikana kama *Common Mans Charter* vilevile haikufaulu na vilevile nchini Kenya utaifa haupo tena. Hii ni mfumo ambayo ilinuiwa kuwaunganisha wananchi na kufanya ugavi wa rasilimali kuwa sawa, hivyo kufeli kwazo

kumezua hali ya mgawanyiko katika nchi husika.Ukabaila ndiyo chanzo cha matokeo haya na viongozi ndio wenye kupalilia mambo hayo.

Mke wake Macho vilevile anauenzi ukabaila. Yeye ndiye mwajiri wake Penzi, na alitarajiwa kwamba kwa sababu ya kazi nzuri aliyoitekeleza kijakazi wake Penzi, angeonyesha hali ya kuridhika na kuifurahia huduma anayoipata.Lakini badala yake anaonyesha ubarakala wazi wazi.Mumewe anapomuuliza mkewe sababu za Penzi kutohusishwa katika safari ya kuzuru Ukwasini, mkewe alijibu, “Hakuna mahali popote ulimwenguni ambapo watu huenda likizoni na watumishi wao.” (uk 173)

Kauli hii ilimgadhabisha macho na kuchochea hasira yake. Kwake alielewa kwamba Penzi hakuwa tu mtumishi, mbali alikuwa pia mlezi, msichana mwenye tabia njema, rafikiye mwanawao Lulu, ambaye alihatarisha maisha yake ili kumnusuru Lulu alipotekwa nyara na wale magaidi. Kwa hivyo ingekuwa jambo la busara na njia ya kutoa shukrani zao kwake Penzi ikiwa angeandamana nao katika likizo yao.

Ama kweli kauli yeyote iliyojaa ukweli na mantiki haina maana mbele ya chuki, ubaguzi na hamnazo, ilibidi Mheshimiwa Meya , Moran wa uketa, Macho wa Tatu kuumeza mrututu. Tabia za unafiki kama hizi ndizo hudhahirika kwa viongozi ambao hujitakia mema wao peke yao huku wakijifanya kuwa ni marafiki ihali ni adui.

#### **4.2.5 Ukabila**

Ukabila ni tatizo kubwa sana ambalo huchangia katika kuzorotesha siasa za nchi nyingi na kutia sumu katika mahusiano ya kawaida baina ya watu wa makabila tofauti tofauti. Ukabila kwa hakika ni kama kidonda-ndugu na husababishwa na kabila la chovya ambalo wakati mwingi ndilo huwa uongozini.

Katika sura ya pili tulishuhudia jinsi nchi tofauti tofauti zilivyoathirika kwa kuenzi ukabila. Watu wenye ubinafsi mwingi wamewaahini wenzao fursa ya kuyastawisha maisha yao, ni kana kwamba walizaliwa peke yao. Ukabila hufanya kazi jinsi kimbunga au upepo mkali unavyokwenda kasi mno na kuleta hasara. Bila shaka anwani ya riwaya hii *Majira ya Tufani* inatupa dhamira (wazo) inayotawala kazi nzima ya mvutano baina ya Watawala na Wataliwa.

Itikadi ni nguzo muhimu katika Uchanganuzi Hakiki Usemi , ni mawazo ambayo watawala na wataliwa wanaamini kwamba matakwa ya wenye uwezo (watawala) kijamii hudumu. Hata hivyo UHU vilevile huweka usemi wazi kwa kuvumbua kwa undani kaida ambazo ni kinzani na ambazo zinaunda ushindani wa itikadi na uwezo katika matini.

Kiongozi katika kazi hii aliye na itikadi za aina hii ni Balozi Prince Dan. Dan ana mawazo ambayo kwake si rahisi kuyageuza. Anaamini kwamba kabila lake la Ukwasini ndilo tu linalostahili yale yote mazuri (watawala na matajiri) ilihali lile la uhasimu (watawaliwa na maskini) hawastahili chochote. Katika hotuba yake, Balozi anatumia maneno haya kueleza ustaarabu wa kabila lake,

Afuataye mafunzo ya dini  
hufanikiwa, Ukwasi ni dini ya  
maendeleo; ni dini ya ustaarabu;  
ni dini ya usasa. Sio kama Uhasimu  
ambayo ni dini ya Ugaidi na  
Ushenzi. ( uk 13)

Mawazo kama haya huipelekea nchi kuamini kwamba baadhi ya makabila hayafai na hata kuifanya nchi kuingia katika vurugu za kikabila. Ni wazi kwamba maneno au lugha, kivyake haina uwezo na hupata uwezo kupitia jinsi ambavyo wale wenye uwezo hutumia lugha hii Van Dijk (1997). Mara nyingi maana au uelewa wa maneno hujitokeza wakati ambapo mazungumzo au maandishi yanamaanisha zaidi ya yale ambayo yanasemwa au kuandikwa. Hii ndiyo sababu ya kuifanya kabila ya uhasimu kutoa fujo na kuvuruga sherehe ya ufunguzi wa Macho Plaza. Jambo hili lilisababisha maafa mengi katika nchi ya Uketa, mali kupotezwa na hata Lulu kutekwa nyara.

Itikadi kama hizi ndizo hasa zinazoendeleza ukabila ili kuwafanya wanyonge wajipate katika hali ya kufadhaisha. Kama ilivyodhihirika imani zenyewe hazina ukweli wowote wa Kisayansi bali ni mawazo fulani ambayo huchangiwa pakubwa na mifumo ya kisiasa na kiuchumi ili kuendeleza umaskini unaosababishwa na wale walio mamlakani.

#### **4.3 Viongozi tofauti tofauti katika riwaya ya *Majira Ya Tufani*.**

Kutokana na uchambuzi wa maudhui kuhusu riwaya hii imedhihirika kwamba kuna baadhi ya viongozi katika jamii ya Wananakada ambao maneno na matendo yao yamedhihirisha unafiki wao, hujuma zao kwa uchumi wa Uketa, na pia matendo yao ambayo hayaakisi maadili ya kijamii. Baadhi ya viongozi hao katika kazi hii ni pamoja na Balozi wa Ukwasini Dan Prince, Meya Wa Nakada Macho wa Tatu, na kamishna wa polisi baina ya wengine.

##### **4.3.1 Balozi Dan Prince**

Balozi ni mtu ambaye hupelekwa na serikali yake katika nchi ya kigeni ili kuwakilisha nchi yake kule. Kwa sababu hii balozi kama kiongozi hutarajiwa kuwa mfano mwema kwa jamii.



Balozi Dan Prince kinyume na matarajio ya Wanauketa, hakuonyesha sifa za kiongozi mzuri tulizozifafanua katika sura ya pili. Badala ya kuwakilisha nchi ya Uketa kama alivyostahili kufanya, yeye ndiye aliyekuwa mstari wa mbele katika kuudumisha utabaka wa Kimataifa. Jambo hili lilidhihirishwa katika utekelezaji wa ulaghai wake.

Tulishuhudia jinsi alivyomshinikiza Mheshimiwa Meya Wa Nakada Macho Wa Tatu katika kuudumisha ukoloni mamboleao. Balozi Dan alijifanya rafiki mkubwa wa Wananakada kwa kuonyesha mshikamano kupitia utandawazi huku akisaidia nchi yake katika kuinyanyasa Uketa. Alijitahidi kuhakikisha kwamba uchumi wa Uketa uliingia katika himaya ya Ukwadini.

Balozi Dan alihakikisha kwamba ufisadi umemea mizizi kwa kumhimiza Meya Wa Nakada kuagiza mali ghafi kutoka Ukwadini kwa gharama ya juu ili wenyewe wafaidike. Alihakikisha maliasali inayopatikana nchini Uketa haikutumika. Hata wasanifu wa jengo la Macho Plaza walitoka Ukwadini eti mataifa yaliyoendelea. Jambo lililoashiria kwamba Wasanifu wa nchi ya Uketa hawajahitimu. Bila shaka hii ilikuwa njia tu ya kuipora nchi inayoendelea ya Uketa.

Balozi Dan aidha alihakikisha kwamba Mahasibu walioonyesha kukiuka maagizo yake Kupitia kwa Meya, wameadhibiwa vikali. Ishara ambayo ilionyesha kwamba bado mkoloni anatawala. Balozi Dan alifanya mambo yake kama ndumakuwili. Alijifanya rafiki mkubwa wa Wanauketa huku akiwahadaa. Tulishuhudia hata akimnyemelea mke wa Meya Macho aliyekiri kwamba ni rafikiye na vilevile mmoja wao kwa sababu ya nyendo zake za Ukwadini alizoziiiga.

Matendo, maneno na nyendo za kiongozi huyu zilisababisha Wananakada kuathirika kwa njia Nyingi.

#### **4.3.2 Meya wa Nakada Macho Wa Tatu.**

Meya ni viongozi waliochaguliwa kusimamia mabaraza katika miji mikubwa. Hao ndio hua wenye kiti wa halmashauri ya miji yao. Mipango yote ya miji hutekelezwa chini ya viongozi hawa. Mambo yanayohusu uchumi na rasilmali za miji huendeshwa chini ya viongozi hawa. Wao ndio husababisha mabadiliko ya miji yao.

Meya wa Nakada, Macho wa Tatu ni kiongozi ambaye hastahili kuwa kiongozi wa Wananakada, badala ya kutoa huduma zitakazowafaidi Wananakada, alitumia uwezo wake kuwadhulumu. Alifanya kile ambacho kilihusu maslahi yake tu, bila kujali umma.

Imedhihirika wazi wazi kwamba Macho ndiye mwanzilishi wa uhasama unaoshuhudiwa kule Uketa. Anasababisha mvutano baina ya Wahasimu na Wakwasi, yaani tabaka la juu na lile la chini. Uongozi hafifu na uliojaa uhafidhina aliutekeleza Meya Macho, ulichangia pakubwa katika kuleta mvutano huo. Hali hii imechangiwa sana na yule Balozi Dan ambaye alionyesha sifa za mabaki ya kikoloni.

Meya huyu alinyakua ardhi ya umma kwa kushinikizwa kufanya hivyo na kiongozi Dan Prince. Alitaka kujinufaisha huku akiwacha jamii ya Uketa ikilalamika. Ufisadi unatekelezwa wazi wazi bila kuficha haja zao. Baada ya Wananakada kutambua wanahadaiwa, Meya alibadilisha mbinu zake. Aliwatumia maafisa wa kiserikali kuwalaghai Wananakada. Nyendo

zake potovu zilisababisha jamii yake kuangamia huku wengi wao wakiaga na wengine kujipata matatani.

#### **4.3.3 Kamishna wa polisi**

Kitengo cha polisi ni asasi muhimu katika jamii yoyote. Wao huhakikisha kwamba usalama na amani zimedumishwa kila wakati na kila mahali.

Kamishna wa polisi katika mji wa Nakada hakuzingatia kazi yake, kwani matendo na maneno aliyotumia kwa Wananakada yalidhihirisha kuzembea kazini na kutenda kinyume na matarajio ya jamii yake. Polisi huyu ndiye hasa anayekibuni kile kikosi maalum cha Operesheni Fukuachapa cha kumsaka Lulu yule mtoto wa Meya wa Nakada aliyatekwa nyara na Wahasimu. Balozi Dan Prince ndiye hasa kinara katika mipango yote.

Katika operesheni yao kikosi hiki kilitumia njia zote mbaya katika kuwadhulumu Wananakada na hasa wale Wahasimu wa Mwembeni kunakoishi kina yahe. Vilio vya wanyonge vilihanikiza na vilevile damu ilitiririka kule Mwembeni na hata wengine kuuawa na polisi kwa kisingizio cha kumsaka Lulu. Hakuna mwanahasimu aliyesazwa katika operesheni hiyo huku wale waliohusika katika utekaji nyara wakinusurika bila hata maficho yao kupatikana yalipokuwa.

Kwa ufupi kamishna na kikosi chake badala ya kutoa ulinzi kwa wananchi na kulinda mali yao, waliwageuka raia na kuwafanyia dhuluma za kila aina. Kiongozi wa aina hii bila shaka hastahili kukiongoza kikosi chochote kwa sababu kikosi chake hakiakisi maadili ya jamii. Ni sharti hatua kuchukuliwa ili kuwadhhibiti viongozi kama hao wanaosababisha jamii kuangamia na huku wakipitisha mafunzo mabaya kwa wadogo wake.

#### 4.4 Hitimisho

Katika sehemu hii tumejishughulisha na uchunguzi na uchanganuzi wa maudhui katika *Majira ya Tufani* (2012). Baadhi ya maudhui ambayo yamejitokeza ni pamoja na ukoloni na ukoloni mamboleo, ufnisadi, udhalimu, ubarakala au ukabaila na ukabila kuihusu jamii ya Wananakada.

Kimsingi maudhui haya yametuwezesha kutambua wahusika (viongozi) wa kazi hii na matendo yao, mitazamo yao, mwonoulimwengu wao na maingiliano yao na Wanauketa kwani wao ndio jira ya matendo na matukio yanayopatikana katika kazi ya Kifasihi. (Wamitilah, 2008:524).

Maneno, matendo na nyendo za viongozi katika riwaya hii yameonyesha kwamba chanzo cha shida zinazoikumba jamii yake zimesababishwa na viongozi wake. Baadhi ya imani za viongozi hao ni kwamba kiasi cha uwezo walio nacho kinawaruhusu kutenda kama wpendavyo dhidi ya wanyonge.

Mwandishi ameonyesha kupitia Macho kwamba viongozi wengi hutumiwa na mataifa yanayoendelea ili kuifisidi nchi yao kwa kuonyesha unafiki wao. Tumeona kwamba mali na pesa nyingi wanazozimiliki wale walio mamlakani ni hakikisho la udhaifu wa sera za uongozi na njia mbaya zinazotumiwa na mataifa mengine ili kuyaangamiza mengine.

Hata hivyo kuna baadhi ya wanyonge wanaojitahidi ili kutetea haki zao. Wanafanya hivi kwa kukaidi na kuzusha uhasama kama njia ya kulipiza kisasi hata kama wengi wao hawafaulu lakini wanajitahidi. Huu ndio uhitaji wa uchanganuzi hakiki usemi unaohimizwa naye Van Dijk kwamba watumie semi zao kujitetea.

# SURA YA TANO

## HITIMISHO

### 5.0 UTANGULIZI

Sura hii imejishughulisha na matokeo ya utafiti wetu, hii ni kulingana na madhumuni ya utafiti kama yalivyodhihirika katika uchunguzi na uchanganuzi wa riwaya zilizoshughulikiwa. Lakini kabla ya kurejelea muhtasari wa matokeo ya utafiti wetu, ni vyema tutaje kwamba riwaya hizi zimewasawiri viongozi kama visababishi vya mabadiliko chanya yanayosababishwa na viongozi wachache, mengi ya mabadiliko katika riwaya hii yamethiirika kuwa hasi.

Mabadiliko haya yameelekea kulandana na yale yanayopatikana katika baadhi ya riwaya za Mbatiah kama vile *Wimbo Mpya* (2004) na *Upotevu* (2005). Mabadiliko kama vile ufisadi, ukoloni, ukoloni mamboleo, unafiki, ukombozi, umaskini, ulaghai, utu na utajiri na mengine. Hii ni dhahirisho kwamba kazi nyingi za mwandishi huyu huchukua mkondo mmoja.

### 5.1 Muhtasari Wa Matokeo ya Utafiti

Katika utafiti huu tumezingatia sana mchango wa viongozi katika jamii. Tumejaribu kuonyesha kwamba mabadiliko yanayoshuhudiwa katika nchi na jamii mbalimbali husababishwa na viongozi. Ingawa viongozi wanastahili kuwa mawakala wa mabadiliko chanya imedhihirika kwamba matatizo hasi yanayozikumba jamii za leo yamesababishwa na viongozi wetu. Jambo lingine lililodhihirika katika utafiti huu ni kwamba jamii kwa kutofurahia mabadiliko mengine walijitetea kwa kukaidi hata ingawa wengi wao hawakufaulu. Mabadiliko haya yamesababishwa na kuwoko kwa uwezo mkubwa wa

kutawala watawaliwa, jambo ambalo limetufanya kukubaliana na Van Dijk kuhusu matumizi mabaya ya uwezo, kupitia usemi kama njia ya kitega uchumi. Na kuchunguza matendo ya viongozi yanayohujumu uchumi wa nchi ndiyo moja kati ya madhumuni ya kazi hii.

Katika sura ya pili ya utafiti wetu mambo ya kimsingi kuhusu matendo ya viongozi yaliyofafanuliwa, baadhi ya sifa za uongozi mbaya zimedhihirika katika riwaya hizi. Hata hivyo kuna baadhi ya sifa chache ambazo zimejitokeza katika kazi hii ambazo hatukuzifafanua. Ni katika riwaya hizi ndimo sifa tofauti tofauti za viongozi zinazoelezea tabia na nyendo zao zimejitokeza. Kwa hivyo ni wazi kwamba tabia na nyendo za viongozi huhujumu uchumi wa nchi.

Madhumuni yetu ya pili katika utafiti huu yalikuwa kutathmini ikiwa matendo ya viongozi yanaakisi maadili ya kijamii, jambo ambalo utafiti wetu umelipinga. Hili limedhihirika kutokana na riwaya tulizozitathmini kwamba viongozi wameilazimisha jamii ya *Vipanya Vya Maabara* kujiingiza katika njia hasi za kujinufaisha. Kama jamii ya *Vipanya Vya Maabara*, viongozi wake wamedhihirisha hali ya kukosa uadilifu na vitawi vyake kama vile nidhamu, uaminifu, bidii na uzalendo.

Vijana ambao ndio kizazi cha kesho na hata viongozi watarajiwa wamejiingiza katika njia mbovu ili kujikimu kimaisha. Wengi wamejiingiza katika ufisadi, ukahaba, wizi wa kimabavu na hata katika uuzaji na utumizi wa madawa ya kulevya jambo ambalo limedhihirika kwa viongozi wao. Tatizo hili bila shaka litaendelea kuwepo ikiwa hapatapatikana suluhu ya dharura kwani matendo na maneno yasiyo ya kuridhisha yatapitishwa kutoka kikazi kimoja hadi kingine. Matendo maovu ambayo yamejikita katika jamii ya leo ni wazi kwamba ndiyo yale yale yanaonekana kwenye viongozi wetu.

Matendo haya ndiyo yanayotuelekeza katika kupambanua hali za unafiki zinazodhihirika katika maneno na matendo ya viongozi ambayo katika utafiti huu umechunguza hali za unafiki zitokanazo na matendo ya viongozi. Katika sura za awali tulidhihirisha sifa za viongozi ambazo zilituelekeza katika kutathmini matendo yao yaliyoonyesha dhuluma na kuzua uhasimu kwa jamii ya riwaya hizi . Ili viongozi hawa waweze kuepuka ghadhabu ya watawaliwa wamedhihirisha hali za unafiki katika maneno na matendo yao.

Viongozi wengi wametumia hali ya kujifanya kuwa ni rafiki huku ikidhihirika wazi wazi kwamba ni adui. Wengi wao wamewaahidi wananchi mambo fulani ambayo hawakutumiza bali hali za jamii zao zilionyesha kutamauka huku wakijipata katika hali ya kurudi nyuma kimaendeleo. Hali kama hizi ndizo zinazoipelekea nchi nyingi kubuni mifumo ya sera na hata kubadilisha vifungu vya katiba ili kuitetea jamii inayoangamia. Bila shaka wananchi hujizatiti vilivyo ili kujaribu kudhibiti uwezo wa viongozi kupitia miswada tofauti, lakini haijatokea kuwa jambo rahisi kwani viongozi ndio watungao na wavunjao zile sheria zinazowadhibiti, jambo linalozisababisha nchi nyingi kurudi nyuma kimaendeleo.

Utafiti wetu ulinuia kujibu maswali yaliyotokana na madhumuni ya utafiti huu. Kwanza, je matendo ya viongozi yanaweza kuhujumu uchumi wa nchi?

Tumbainisha kutokana na data katika riwaya hizi mbili kwamba viongozi kwa kiasi kikubwa wamechangia mno katika kusababisha mabadiliko ya riwaya hizi tumeonyesha jinsi matendo yao yanavyohujumu uchumi wa nchi kwa kushiriki katika ufiisadi, ubepari, ukabila na baina ya viongozi wametumia uwezo wao ili kutekeleza hujuma kwa nia ya kujinufaisha wao wenyewe.

Imedhihirika kwamba kuwafanya wenzao kuwa vyombo vya kufanyia tafiti zao kumeigeuza jamii zao kuwa maskini na hata kupoteza pesa nyingi katika miradi isiyofaa. Aidha matendo yao yamekiangamiza kizazi cha kesho katika kuwafanyia vijana majaribio ya utafiti.

Swali la utafiti huu la pili kwamba, je, matendo ya viongozi huakisi maadili ya kijamii? Lilijiibiwa kwa kubainisha jinsi matendo yanavyopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Utafiti huu umedhihirisha kwamba nyendo na matendo mabaya yanayoshuhudiwa katika jamii za riwaya hizi ndiyo yale yale yanayoshuhudiwa kutoka kwa viongozi. Nyendo za ufisadi, ubakaji, unafiki, ulaghai baina ya mengine yamedhihirisha kwamba matendo ya viongozi bila shaka hayaakisi maadili ya jamii.

Katika kulijibu swali la tatu kwamba, je, maneno na matendo ya viongozi aghalabu hudhihirisha unafiki wao? Utafiti umedhihirisha kwamba maneno na matendo yaliyowagadhabisha Wananakada na vilevile Wanauketa hadi kuzipelekea jamii hizi kukaidi, viongozi walitumia njia za kuwahadaa ili kuiepuka gadhabu yao. Kazi hii ilibainisha njia potovu walizotumia kuwazima wananchi zilizohusisha hata kutekeleza mauaji ili kuficha ukweli.

Matendo haya yalidhihirisha unafiki wao lakini ili jamii ifaulu katika kudhibiti nguvu na uwezo mkubwa ulio na viongozi wa jamii hizi ni lazima kujitetea kwa kupinga na kukaidi kuhusu matendo, maneno na hata nyendo potovu zinazoibuliwa na viongozi ambao tumedhihirisha kwamba ndio visababishi vya mabadiliko katika riwaya za *Vipanya vya Maabara na Majira ya Tufani*.



Hili bila shaka ni tatizo linalozikumba nchi nyingi duniani na hasa katika Afrika ya Mashariki. Tumeshuhudia matatizo yayo hayo nchini Kenya na itatulazimu kutia bidii ili kujinusu na janga hili

## **5.2 Tafiti za baadaye**

Utafiti wa baadaye unaweza kuchanganua namna baadhi ya waandishi wanavyosawiri matatizo katika jamii zao kwa kutumia tanzu mbali mbali.

## MAREJELEO

Amaoko, K. Y. (2000). *EAC, Executive Secretary's Address at the ECA: Conference of Ministers*. Addis Ababa, Ethiopia.

Castro, F. (1968). *History Will Absolve Me*. London: Grossman Publishers.

Colin, L. (1995). *Mwalimu: The Influence of Nyerere* Trenton. African World Press

Denied, S. (1967). *The Arusha Declaration and TANU's Policy on Socialism and Self Reliance*. Tanzania: Publicity Section Publishers..

Fairclough, N. (1989). *Language and Power*. London: Longman.

\_\_\_\_\_ (1993). *Discourse and Social change*. Cambridge: Polity Press.

Fairclough, N. L. and Wodak, R. (1997). Critical Discourse Analysis; in T.A. Van Dijk(Whr). *Discourse studies: A Multidisciplinary Introduction, Vol. 2*. Discourse as social interaction. London: Sage Publishers.

Granford, P. Julius Nyerere: *Reflections on the Legacy of his Socialism*. Canadania Journal of Africa Studies 33.

Himbara, D. (1994). *Kenyan Capitalists, the state and Development*. Nairobi: East Africa Publishers Ltd.

Kiongera, K. J. (2012). Mchango Wa Vijana Kuleta Mabadiliko Chanya Katika Tamthilia Teule Za Kiswahili. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili: Chuo Kikuu Cha Nairobi (ambayo haijachapishwa).

Lazar, M. (Mhr) (2005). *Feminist Critical Discourse Analysis: Gender, Power and Ideology in Discourse*. Houndsmills, UK: Palgrave MacMillan.

Makgoba, M. W. (1997) *Makoko: The Makgoba Affair- A Reflection on Transformation*.

Florida: Vivlia

Manoti, J. N. (2012). *Dhamira Ya Uozo na Athari Zake Kwa Jamii, Katika Riwaya ya*.

*Upotevu: tasnifu ya shahada ya Uzamili: Chuo Kikuu Cha Nairobi.*

Haijachapishwa.

Marx, K. and Engels, F. (1968). *The Communist Manifesto*. Penguin Books.

Mbatiah, M. (2004). *Wimbo Mpya*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

\_\_\_\_\_ (2005). *Upotevu*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

\_\_\_\_\_ (2007). *Vipanya Vya Maabara*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

\_\_\_\_\_ (2012). *Majira Ya Tufani*. Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Mnara Wa Mlinzi (2013). *Kwa nini Ulimwengu Hauna Umoja*. Mchapisho Kwenye Mtandao.

Mohamed, A. S. (1978). *Asali Chungu*. Kampala Uganda: Longhorn Publishers (U) Ltd.

\_\_\_\_\_ (1980). *Utengano*. Kampala Uganda: Longhorn Publishers (U) Ltd.

\_\_\_\_\_ (1980). *Dunia Mti Mkavu*. Kampala Uganda: Longhorn Publishers (U) Ltd.

Mugambi, E. K. (1983). *Kilio Cha Wanyonge Katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed:*

*Tasnifu ya Shahada Ya Uzamili: Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)*

Mwanasheria Mkuu, (2010). *Katiba Ya Jamhuri Ya Kenya*. Nairobi: International Institute for  
Legislative Affairs.

Naliaka, E. K. (2012). *Uhakiki Wa Hali Ya Vijana Katika Riwaya Ya Vipanya Vya Maabara:*

*Tasnifu Ya Shahada ya Uzamili. Haijachapishwa.*

- Njogu, k. na Chimera, R. (2011). *Ufundishaji Wa Fasihi- Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Ochola, A.S. (2007). *Leadership and Economic Crisis in Africa*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- O'Connor, D.E. (2004). *The Basics of Economics*. U.S.A: Greenwood Publishing Group.
- Oginga, O. (1967). *Not yet uhuru*. Kenya: East African Publishers Amazon .com
- Plaut, M. (2012). "Africa's Bright Future" BBC News Magazine.
- Porter, P.W. (2006). *Challenging Nature: Local Knowledge, Agrosience and Food Security in Tanga*. U.S.A: University of Chicago Press.
- Pratt, C. (1999). *Julius Nyerere: Reflections on the Legacy of his Socialism*. Canadian Journal of African Studies 33.
- Ramose, M. B. (1998). Forward in *S. Seepe (ed) Black Perspective(s) on Tertiary Institutional Transformation*. Johannesburg: Vivlia.
- Reisigl, M. and Wodak, R. (2001). *Discourse and Discrimination: Rhetorics of Racism and Antisemitism*. London: Routledge
- Rotchild, D. (1969). *Ethnic Inequalities in Kenya*. London: Cambridge University Press.
- Ronald, E.W. and Edgar, S. (1964). *Corruption in Developing Countries*. London: George Allen and Unwin Ltd.
- Sandbrook, R. (1958). *The Politics of Africa's Economic Stagnation*. London: Cambridge University Press
- Sidney, L. J. (2011). *Ni Wapi Tunakwenda: Hip Hop Culture and the Children of Arusha*. London: M1: Plut Press
- Stapenhurst, R. and Kpundeh, S. J. (1999). *Curbing Corruption toward a Model for building National Integrity*. Washington D.C. World Bank Statistics.

- Tim, O.(1988) *Africa Leadership Forum: The Challenges of Leadership in Africa Development*. Nigeria: Ota
- Thomas, P. (1991). *Tanzania's Travail: Lessons in Improving American aid to The Third Third World*. The Heritage Foundation.
- Van Dijk, T.A. (1998A). *Critical Discourse Analysis*. Available:  
<http://www.hum.Uva.nl/teum/ada.htm> (1/5/2014)
- \_\_\_\_\_ (2008). *Discourse and Power*. New York: Palgrace MacMillan.
- Wa Mberiah, K. (2001). *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publications LTD.
- \_\_\_\_\_ (2004). *Maua Kwenye Jua La Asubuhi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.
- Wamitila, K. W. (2003). *Pango*. Nairobi: Focus Publication Ltd.
- \_\_\_\_\_ (2008). *Kanzi Ya Fasihi Misingi Ya Uchanganuzi Wa Fasihi*.Nairobi:  
 Vide-Muwa Publishers Limited.
- \_\_\_\_\_ (2009). *Seserumbe*. Nairobi: Video-Muwa Publishers Ltd.
- Were, G.S. (1983). *Leadership and Undevelopment in Afrika*. Nairobi: Gidions Were Publishers.
- Wodak, R. (1997). *Gender and Discourse: Sage Studies in Discourse*. London. Sage Publishers.
- Wodak, R. and Ludwig, C. (1999). *Challenges in a Changing World*. Vienna: Passagen Ver:ag.
- Wodak, R. and Meyer, M. (Whr) (2001). *Methods of Critical Discourse Analysis*. London: Sage Publishers.
- Woodrow, W. (2005). *Challenges And Change in Uganda*. Washington D.C:  
 Woodrow Wilson International Center for Scholars.
- Yonas, D. (1988). *Subsidizing Tragedy: The World Bank and New Colonialism*. The Heritage Foundation.